# Nipashe

Jumamosi Aprili 15, 2023 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0581281

www.ippmedia.com

MWANGA WA JAMII

The Guardian digital nipasheTZ nipasheTZ nipasheTZ 0745 700710 LIKE & FOLLOW US





UKURASA 11


MID WEEK JACKPOT!
TZS. 544,830,140
KWA TZS. 1000 TU!
SCAN HAPA KUPAKUA APP YETU!
SportPesa.CO.TZ
PIGA *150*87#




**Kiwanda** chapigwa faini kwa madai ya uchakachuaji wa saruji

UKURASA 3

# KICHEKO TAMISEMI



Angellah Kairuki

UKURASA 2

**MAPATO, MATUMIZI**

Fungu lapaa kutoka Tril. 9.04/- 2022/23 hadi Tril. 9.144/-



**UCHAGUZI MITAA**

Mikakati kufanikisha uchaguzi katika halmashauri zote 184.



**UNUNUZI WA BOTI**

Boti kununuliwa maeneo yenye shida ya usafiri majini.




**MWENDOKASI**

Mabilioni yatengwa kuufikisha mradi Gongo la Mboto.



**SOKO LA KARIAKOO**

Bil. 1.68/- kukarabati soko lililoungua Kariakoo



**HUDUMA ZA AFYA**

Ujenzi na ukarabati wa zahanati, vituo vya afya watengewa mabilioni.





**KAYA MASIKINI**

Fungu maalum latengwa kufuatilia utekelezaji miradi TASAF

**ELIMU BURE**

Bajeti Elimu Bila Malipo nyongeza asilimia 15



**UFANISI TARURA**

Bilioni 710/- zatengwa ujenzi, ukarabati barabara vijijini na mijini.



**SHULE NA LISHE**

Shule kongwe msingi na sekondari zina fungu kuzing'arisha, lishe duni yawekewa mkakati



**UPANDISHAJI VYEO**

Mamlaka kuratibu upandishaji vyeo watumishi



## Mtoto aliyepotea siku mbili akutwa karibu na simba

UK.3

## Vifaa tiba mil. 500/- vyadaiwa kuibwa hospitali ya wilaya

UK. 2


MICHEZO SIMBA, YANGA ZACHANGA KARATA UK.24

MAONI, KATUNI UK.6



Askofu wa Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT), Dayosisi ya Karagwe, Dk. Benson Bagonza (wa pili kushoto), akiwa na waandishi wa habari waandamizi, Absalom Kibanda (kushoto), Nevile Meena (kulia) na Jesse Kwayu, wakionyesha kitabu kijulikanacho kwa jina la "I AM THE STATE", baada ya kukizindua jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: JUMANNE JUMA.**

# Mwaka wa kicheko TAMISEMI

**Na Godfrey Mushi,**
DODOMA

NI kicheko TAMISEMI. Ndicho kinachoweza kuelezwa kutokana na mikakati iliyowekwa na serikali katika kutekeleza majukumu ya Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) kwa mwaka ujao wa fedha.

Hotuba ya makadirio ya mapato na matumizi ya ofisi hiyo iliyowasilishwa bungeni jijini hapa jana na Waziri wake, Anjellah Kairuki, inaonyesha serikali imeelekeza Sh. trilioni 9.144 kwa ajili ya utekelezaji wa shughuli za ofisi hiyo.

Miongoni mwa maeneo yaliyopewa kipaumbele ni uchaguzi wa serikali za mitaa wa mwakani uliopangwa kufanyika kwenye vijiji 12,318, mitaa 4,263 na vitongoji 64,361 katika halmashauri zote 184 nchini.

Kwa mujibu wa Kairuki, kwa mwaka wa fedha 2023/24, fungu la utekelezaji Mpango wa Elimu Msingi bila Ada, maarufu Elimu Bure, ni Sh. bilioni 399.64. Hilo ni ongezeko la Sh. bilioni 53.15 (asilimia 15.34) kulinganishwa na bajeti ya Sh. bilioni 346.49 iliyoidhinishwa mwaka 2022/23.

Waziri Kairuki alisema ongezeko hilo linatokana na wanafunzi wa kidato cha tano na sita kujumuishwa katika mpango huo.

Mpango wa kaya masikini, umetengewa Sh. milioni 150 (fedha za nje) kwa ajili ya TAMISEMI kwa kushirikiana na Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF) kusimamia utekelezaji wa miradi inayohusu kupunguza umasikini ngazi ya kaya katika mikoa 26 ya Tanzania Bara.

Alisema miradi ya matengenezo ya barabara inayotekelezwa na Wakala wa Barabara za Mijini na Vijijini (TARURA), imetengewa Sh. bilioni 710.316 fedha za ndani nas kati ya fedha hizo, Sh. bilioni 257.03 ni za Mfuko wa Barabara; Mfuko Mkuu wa Serikali Sh. bilioni 127.5 na tozo ya mafuta Sh. 100 kwa lita ambayo ni Sh. bilioni 325.77.

Mradi wa Kuboresha Elimu ya Awali na Msingi (BOOST), umetengewa Sh. bilioni 20.259 (fedha za nje). Ofisi ya Rais-TAMISEMI, kupitia mradi huo, itanunua na kusambaza vifaa vya Tekonolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) katika shule za msingi 200. Mpango huo unalenga kuboresha ujifunzaji wa wanafunzi na Mafunzo Endelevu ya Walimu Kazini (MEWAKA), kutekeleza Mpango wa Shule Salama kwenye shule za msingi 2,500, kununua na kusambaza vifaa vya kufundishia na kujifunzia elimu ya awali kwenye shule za msingi 3,000 na kutoa mafunzo kwa walimu wa elimu ya awali.

Pia, kufanya ufuatiliaji na tathmini ya ujenzi wa vyumba vya madarasa 4,730 na matundu ya vyoo 3,010; Mafunzo Endelevu ya Walimu Kazini (MEWAKA); uandikishaji wa wanafunzi; ufundishaji na ujifunzaji wa elimu ya awali na msingi katika halmashauri zote 184.

Kwa programu ya kuboresha chakula na lishe kuboresha afya kwa watoto wanaoishi kwenye mazingira hatarishi na wanawake (WPP & NI), Waziri alisema inaomba kutengewa Sh. 158,481,653 ambazo ni fedha za nje.

Pia alisema Wakala ya Mabasi Yaendayo Haraka Dar es Salaam (DART), umeomba kuidhinishiwa Sh. bilioni 3.03 kwa ajili ya matumizi ya kawaida. Kati ya fedha hizo, Sh. bilioni 2.3 ni kwa ajili ya mishahara na Sh. milioni 731.21 ni kwa matumizi mengineyo pamoja na kujenga kilomita 20 ili kuupeleka mradi Gongo la Mboto.

Tume ya Utumishi wa Walimu, inaomba kuidhinishiwa Sh. bilioni 17.20, kwa ajili ya matumizi ya kawaida na maendeleo, yakijumuisha kuwapandisha vyeo walimu wenye sifa baada ya kupata vibali kutoka kwenye mamlaka husika.

### KARIAKOO

Kuhusu mikakati ya kuimarisha huduma kwenye Shirika la Masoko ya Kariakoo, Waziri alisema shirika hilo linaomba kuidhinishiwa Sh. bilioni 1.68 kwa ajili ya matumizi ya kawaida. Kati ya fedha hizo, Sh. milioni 747.54 ni kwa ajili ya mishahara na Sh. milioni 938.44 matumizi mengineyo.

Alisema shirika litaendelea na ujenzi wa soko jipya na ukarabati wa soko lililoungua unaotarajiwa kukamilika Oktoba mwaka huu.

### MAPATO YA NDANI

Katika mwaka wa fedha 2023/24 Ofisi za Wakuu wa Mikoa, Halmashauri na Taasisi zilizo chini ya Ofisi ya Rais - TAMISEMI zimepanga kukusanya maduhuli na mapato ya ndani yenye jumla ya Sh. trilioni 1.19.

Kati ya fedha hizo, Sh. bilioni 55.14 zimepangwa kukusanywa na taasisi zilizo chini ya Ofisi ya Rais - TAMISEMI, Sh. milioni 261.89 zitakusanywa na Ofisi za Wakuu wa Mikoa na Sh. trilioni 1.14 zitakusanywa na halmashauri.

### MABILIONI VITUO VYA AFYA

Katika makadirio hayo, Waziri Kairuki, alisema sekta ya afya itaendeleza ujenzi wa hospitali 41 za Halmashauri, ambapo Sh. bilioni 30.29 zimetengwa. Pia katika kufanya ukarabati wa hospitali kongwe za halmashauri 31, Sh. bilioni 27.9 zimetengwa; lakini pia kuna ujenzi wa vituo vya afya 16 na ukamilishaji wa vituo vya afya sita, ambapo Sh. bilioni 9.54 zimetengwa. Aidha, Sh. bilioni 18.80 zimetenwa kwa aliji ya kurarabati wa zahanati 376 katika halmashauri.

### UNUNUZI WA BOTI

Waziri Kairuki alisema katika mwaka wa fedha wa 2023/24, TAMISEMI imetengewa Sh. bilioni 1.5 kwa ajili ya ununuzi wa boti nne katika halmashauri za Wilaya za Ludewa, Buchosa, Nyasa na Sumbawanga ili kuimarisha doria, ulinzi na ukusanyaji wa mapato ya ndani.

### MAGARI YA MA RC,DC

Kwenye bajeti hiyo, Waziri Kairuki aliainisha kuwa katika mwaka 2023/24, TAMISEMI imetengewa Sh. bilioni 16.58 kwa ajili ya ununuzi wa magari 81 katika ofisi za wakuu wa mikoa yakiwamo matano ni ya wakuu wa mikoa, mawili ya makatibu tawala wa mikoa na magari 74 ya wakuu wa wilaya.

# Vifaa tiba mil. 500/- vyadaiwa kuibwa katika hospitali ya wilaya

**Na Vitus Audax**

VIFAA tiba vyenye thamani ya Sh. milioni 500 vinadaiwa kuibwa katika mazingira ya kutatanisha katika Hospitali ya Wilaya Bunda mkoani Mara, huku baadhi ya milango ikikutwa wazi.

Kutokana na tukio hilo, Mganga Mkuu wa Wilaya hiyo (jina halijatajwa) anashikiliwa kwa ajili ya uchunguzi zaidi na Mganga Mfawidhi ametakiwa kuripoti kwa mwajiri wake, wakati taratibu zingine za kisheria zikiendelea.

Upotevu huo ulibainika Jumamosi iliyopita baada ya Mganga Mfawidhi wa Hospitali hiyo, Dk. Ally Abdallah, kufika hospitalini hapo na kukuta vifaa ambavyo vilifikishwa mwaka jana havipo.

Dk. Abdallah alisema alikuta baadhi ya milango imefunguliwa na vifaa zikiwamo komputa mbili, ultra sound na vifaa vingine vyenye thamani ya Sh. milioni 500 vikiwa vimeibwa.

"Kumtambua mhusika wa wizi huu ni vigumu kwa sababu sikumwona yeyote wakati huo. Inaonekana ni mtu wa karibu na sisi kutokana na mazingira ya wizi yalivyokuwa," alisema.

Baadhi ya wananchi na majirani wa hospitali hiyo akiwamo Toronto Makongoro, walisema kabla ya tukio hilo, waliona gari la Mganga Mfawidhi likizunguka eneo la hospitali hiyo nyakati za usiku, na kusimama mbali kidogo na hospitali.

Walidai kuwa hospitali hiyo ambayo imeanza kujengwa tangu mwaka 2019, imekuwa na ubadhirifu mkubwa ikiwa ni pamoja na wizi wa vifaa vya ujenzi, hali ambayo ilisababisha kutokukamilika kwa zaidi ya miaka minne na kuwatuhumu watumishi kuhusika na wizi.

Diwani wa Nyamuswa, Ibrahim Mganga, alisema mazingira ambayo wanaambiwa vifaa hivyo vimeibwa yanawatia wasiwasi.

"Haiwezekani, kuna mtu anatoka hapa hapa alikuwa na ufunguo akafungua na kuiba kisha, akafunga," alisema.

Baada ya kupokea malalamiko ya wananchi kuhusu wizi huo, Mkuu wa Wilaya ya Bunda, Dk. Vicent Naano, alisema wamemkamata Mganga Mkuu wa Wilaya hiyo kwa ajili ya uchunguzi zaidi na kumtaka Mganga Mfawidhi, kuripoti kwa mwajiri wake, ili taratibu nyingine za kisheria ziendelee.

Dk. Naano alisema hospitali hapo atapelekwa mganga mfawidhi mwingine haraka iwezekanavyo, wakati taratibu za kuvipata vifaa hivyo, zikiendelea kufanyika.

"Hapa wizi haujafanyika, ila mmeamua kuchukua vifaa hivi, wewe nenda karipoti kwa mwajiri wako huku wakati kesi yako ikiwa inakusubiri mahakamani na bado una kesi nyingine, tutamleta Mganga mwingine kwa ajili ya hospitali hii," alisema Dk. Naano.



Mkuu wa Jumuiya ya Shia Ithna'ashariyyah Tanzania, Shekhe Hemed Jalala (wa pili kushoto), akiongoza matembezi ya hiyari ikiwa ni siku ya Quds ambayo inaadhimishwa Ijumaa ya mwisho wa mwezi wa Ramadhani, yaliyoanzia Ilala Boma hadi Kigogo Posta, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Mtoto aliyepotea akutwa karibu na kundi la simba

**Na Jenifer Gilla**

MTOTO Justine Kilusu, mwenye umri wa miaka mitano, kutoka Kijiji cha Kakoi, babati mkoani manyara, aliyepotea kwa siku mbili amekutwa katika Hifadhi ya Tarangire mita 200 karibu na kundi la simba.

Baba wa mtoto huyo, Samweli Kilusu, alisema mwanawe alipotea Jumapili iliyopita, saa 7:00 mchana alipokuwa na wenzake pamoja na kaka yake wakilisha mifugo katika pori la jumuiya lililo karibu na eneo wanaloishi.

Alisema taarifa za kupotea kwa mtoto wao walizipata kupitia kaka yake baada ya kurudi nyumbani akitoka safari ya kikazi Moshi, Kilimanjaro na mama yake akitokea mnadani.

Kilusu alisema baada ya kupokea habari hizo, walitoa taarifa kwa mtendaji wa mijiji kwa lengo la kuongeza nguvu ya kumtafuta.

"Siku hiyo tulimtafuta kuanzia saa 1:00 jioni hadi saa 4:00 usiku bila mafanikio. Jumatatu (Aprili 10), mwenyekiti alipiga mbiu kubwa wanakijiji wa hapa na vijiji vya jirani wakajitokeza, tukaingia porini kumtafuta kuanzia 12:00 hadi saa 4:00 usiku bila mafanikio," alisema.

Siku iliyofuata, majira ya saa 1:00 jioni, alisema wakati wakiendelea na msako katika mapori mengine, walipokea taarifa kutoka kwa askari wa Hifadhi ya Tarangire, katika kijiji cha Vilima Vitatu kuwa kuna mtoto ameokotwa hifadhini na kukuta ni mwanawe.

Kilusu alisema mtoto wake alimsimulia kuwa akiwa porini alikutana na fisi na alipotaka kumshambulia akamtisha na fimbo akakimbia na baadaye aliwaona simba wakiwa mbali kidogo na eneo alikokuwa.

"Ninamshukuru Mungu sana afya ya mtoto inaendelea kuimarika taratibu. Nilishakata tamaa kwa kuwa mapori haya yana wanyama wengi wakali wakiwamo simba, fisi na tembo ambao wangeweza kumdhuru," alisema.

Mwenyekiti wa kijiji hicho, Loishiye Elias, alisema baada ya kupiga mbiu kubwa walijitokeza zaidi ya watu 500 wakiwamo vijana kutoka vijiji vya Mswakini, Olasiti, Minjingu na Kakoi, askari wa hifadhi na kampuni za utalii na msako wa usiku na mchana ulifanyika kwa siku mbili.

Jumanne wiki hii, majira ya saa 1:00 jioni, alisema alipigiwa simu na askari mmoja wa Hifadhi ya Tarangire kuwa wamemwokota mtoto huyo ndani ya hifadhi akiwa anavuka barabara kwa shida, mita 200 lilipokuwapo kundi la simba.

Alisema askari hao alimpa huduma ya kwanza ikiwamo chakula, kumwogesha na kumbadilisha nguo kisha wakampeleka kijijini lakini kutokana na hali yake kuwa dhaifu, alipelekwa katika Hospitali ya Ngaiti.

Elias alisema vipimo vya daktari vilionyesha mtoto huyo hana tatizo kubwa zaidi ya sukari kushuka kutokana na kutokula chochote kwa muda mrefu.

"Madaktari walishauri aendelee kukaa hospitalini kwa saa kadhaa zaidi ili kama kuna tatizo lolote litakalojitokeza wamsaidie. Kwa hiyo alikaa hadi leo (juzi) ndipo akaruhusiwa kurudi nyumbani baada ya afya yake kuimarika," alisema.

Chifu wa Kitongoji wa Eluway, Leteiva Loburu, alisema kilichomsaidia mtoto huyo kutodhuriwa na wanyama wakali porini ni kunatokana na wanavyoishi vizuri na wanyama hao bila uadui.

"Kutokana na elimu tuliyopewa na wahifadhi ya namna ya kuishi vizuri na wanyama, sasa hivi hakuna uadui. Tunaishi nao vizuri na ni kawaida kupishana na simba, tembo na twiga, kila mmoja akaenda njia yake," alisema.

***Habari hii imefanikishwa kwa ufadhili wa mradi wa USAID Tuhifadhi Maliasili unaotekelezwa na Chama cha Waandishi Habari za Mazingira (JET).**

# Kiwanda chatozwa faini uchakachuaji saruji

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

SERIKALI imekichukulia hatua za kisheria kiwanda cha Maweni Limestone Limited kinachozalisha saruji aina ya Hauxin mkoani Tanga kutokana na malalamiko ya watumiaji wa bidhaa hiyo kuhusu upungufu wa uzito wa bidhaa hiyo.

Naibu Waziri wa Uwekezaji, Viwanda na Biashara, Exaud Kigahe aliyasema hayo jijini hapa alipokuwa akizungumzia mwenendo wa bei za bidhaa muhimu nchini kwa mwezi Aprili mwaka huu.

Alisema mmiliki wa kiwanda hicho amekiri kosa hilo na amechukuliwa hatua za kisheria ikiwa ni pamoja na kulipa faini na kupewa maelekezo mengine ikiwemo kufanya marekebisho ya mapungufu yaliyojitokeza.

Kigahe alifafanua kuwa endapo mtu huyo atakuwa amekiri kosa, sheria imempa mamlaka Mkurugenzi Mkuu wa Wakala wa Vipimo kufifisha kosa na kumtoza faini isiyopungua Sh. 100,000 na isiyozidi Sh. milioni 20.

"Sheria hii imetoa adhabu ya jumla kwa mtu ambaye atakuwa ametenda kosa chini ya sheria hii na ni mkosaji wa mara ya kwanza, akitiwa hatiani mahakamani, basi atawajibika kulipa faini isiyopungua Sh.300,000 na kiasi kikisichozidi Sh. milioni 50 au kifungo kisichozidi miaka miwili au vyote kwa pamoja.

"Endapo mtu huyu ni mkosaji wa mara ya pili akitiwa hatiani atawajibika kulipa faini isiyopungua Sh. 500,000 na isiyozidi Sh. milioni 100 au kifungo kisichopungua miaka mitano au vyote kwa pamoja," alisema.

Alibainisha kuwa kifungu namba 41(a) na (b) cha Sheria ya Vipimo, Sura ya 340, kinatoa katazo kwa mtu yeyote kuuza bidhaa yoyote iliyo chini ya uzito, kipimo au namba kama inavyohitajika kwa mujibu wa sheria.

"Sheria hii pia inatoa katazo kwa mtu yeyote katika ufanyaji biashara kutoa taarifa za uongo juu ya bidhaa yoyote kuhusu uzito, kipimo, namba, geji au kiwango. Endapo makosa haya yatafanyika, wote watakuwa wametenda kosa kwa mujibu wa sheria hii,"alisema.

Pia alisema kwa mwenye duka anajukumu la kuhakiki kila bidhaa anayouza kabla ya kumuuzia mlaji wa mwisho na kujiridhisha kuwa bidhaa husika ipo katika hali inayotakiwa kulingana na matakwa ya sheria.

Naibu Waziri aliwataka wazalishaji wa bidhaa za viwandani kuongeza jitihada za uzalishaji wa bidhaa kwa ubora unaohitajika sokoni na kwa kufuata sheria, kanuni na taratibu zilizowekwa ili kukabiliana na mfumuko wa bei za bidhaa mbalimbali.

Kuhusu mwenendo wa bei, Naibu Waziri alisema bei za mazao na bidhaa za chakula zimeshuka kutoka asilimia 0.8 hadi 0.7 huku bei za vifaa vya ujenzi zimeendelea kupanda kutokana na kuongezeka kwa matumizi ya bidhaa hizo.

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA UJENZI, NA UCHUKUZI**

Simu: +255 26 2324455
Fax: +255 26 2323233
Barua Pepe: ps@mow.go.tz
Tovuti: www.mwtc.go.tz

Mtaa wa Mtumba,
S.L.P. 2888,
40470DODOMA,
07 - 10 - 2022

## TAARIFA KWA UMMA

1. Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi (Sekta Ujenzi) inapenda kuutaarifu umma kuwa siku ya Alhamisi tarehe 20-04-2023 kampuni ya Mainline Carriers Ltd itasafirisha Mizigo yenye vipimo vikubwa kutoka Dar-Es-Salaam Port kuelekea Kilombero kupitia Mikumi, gari hizo zina namba za usajili:

T 460 DYG/ T 879 EAU
T 681 DUB / T 881 EAU
T 482 ECF / T 568 EAZ
T 973 DTN / T 572 EAZ

2. Gari hilo lina vipimo vifuatavyo:
Urefu - mita 25.00 Upana - mita 5.10 Kimo - mita 5.60

3. Njia itakayotumika: Dar-Es-Salaam, hadi Kilombero kupitia Mikumi, gari itasafiri muda wa mchana tu (Kuanzia saa 12:30 Asubuhi mpaka saa 12:00 Jioni)

**Tunaomba radhi kwa usumbufu utakaojitokeza**

HABARI KITAIFA

# Waziri aridhia MSD kununua maji dripu, vifaa tiba kampuni za ndani

**Na Godfrey Mushi,** DODOMA

WAZIRI wa Afya, Ummy Mwalimu, ameridhia Bohari Kuu ya Dawa (MSD), kuanza kununua kwa asilimia 50 maji ya dripu na vifaa tiba vinavyozalishwa na kampuni za kizalendo za Kairuki Pharmaceuticals Industry Ltd (KPIL) na Alfa Pharmaceutical Production Plant.

Akizungumza jana na wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Maendeleo ya Jamii, iliyotembelea na kukagua MSD Kanda ya Dodoma, Waziri Ummy alisema viko viwanda viwili nchini vya kuzalisha maji ya dripu, ambavyo vimeihakikishia serikali kuwa vina uwezo wa kukidhi soko la ndani.

"Maelekezo ninayoyatoa kwa MSD hapa ni kwamba kuanzia sasa tutanunua maji ya dripu katika viwanda vyetu vya ndani lakini na wale wazalishaji tusije tukazuia kuingiza za nje, tunaanza na asilimia ya soko ya mahitaji. "Tutaanza kidogo kidogo kuchukua kwa asilimia 50. Naanza kuona matumaini kwa MSD, kwamba tunakwenda vizuri, tutakwenda sasa vizuri endapo kila mtu atatimiza wajibu wake," alisema.

"Naomba sana waheshimiwa Wabunge tuisimamie, asilimia 33 ya fedha za mfuko wa afya wa pamoja inapaswa kwenda kwenye dawa. Sasa kuna hizi pesa ambazo hazirudi MSD inapokwenda kwenye Halmashauri, tunataka hii pesa tuipate juu kwa juu," aliongeza.

Mwenyekiti wa Kamati hiyo, Stanslaus Nyongo, akizungumza baada ya kukutana na menejimenti ya MSD, alisema kazi wanayoifanya (MSD) ni kubwa na inahitaji utaalamu wa hali ya juu.

"Kazi ya kutunza dawa, ununuzi na usambazaji wa dawa, si sawa na bidhaa nyingine. Ni kitu ambacho tunatambua jinsi mnavyopambana. Sisi kama wawakilishi wa wananchi, tutaendelea kuwapima kwa kitu kimoja, upatikanaji wa dawa basi. "Tunataka kuona dawa zinapatikana kwa wakati, zinapatikana kituo cha afya, kwenye hospitali, hicho ndio kipimo chetu. Tunatambua changamoto lakini kwa niaba ya kamati hii, tunachokiona Wabunge sasa hivi kuna maboresho makubwa yaliyopatikana," alisema.

"Changamoto bado zipo lakini kwa mikakati mliyotuonesha hapa, tunategemea kwamba sisi tutaendelea kushirikiana bega kwa bega kuhakikisha kuwa hiyo mikakati mliyoipanga kukabili changamoto za upatikanaji dawa, tunafikia malengo tuliyokusudia," alisisitiza.

Aidha, Nyongo aliishauri Wizara ya Afya, kufanya upembuzi yakinifu ambao ni sahihi kwenye suala la uzalishaji.



Shekhe Mkuu wa Tanzania, Mufti Dk. Abubakar bin Zubeir (kushoto), Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya Biashara Tanzania Sabasaba Moshingi (watatu kushoto), wakiwaongoza wateja pamoja na wafanyakazi wa benki hiyo katika futari uliyoandaliwa na benki hiyo jijini Dar es Salaam juzi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Serikali yasikia kilio Diaspora

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

Bunge limeelezwa kuwa serikali imeamua kuwapa hadhi maalum Diaspora na kwa sasa inakamilisha tararibu ili hivi karibuni waanze kupatiwa hadhi hiyo.

Aidha, serikali imesema iko mbioni kukamilisha mfumo wa kidigitali wa uandikishaji Diaspora ifikapo Juni, mwaka huu.

Naibu Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Balozi Mbarouk Nassor Mbarouk, aliyasema hayo bungeni jana alipokuwa akijibu swali la nyongeza la Mbunge wa Mikumi (CCM), Dennis Londo.

Mbunge huyo katika swali lake alisema kwa kuwa serikali imekiri mchango mkubwa wa Diaspora ni wakati sasa wa kuondoa vikwazo na kueleza Bunge mchakato wa uraia au hadhi maalum umefikia wapi.

Akijibu swali hilo, Balozi Mbarouk alisema: "Kuhusu kuondoa vikwazo hili ni kweli kwa kutambua mchango mkubwa wa Diaspora katika maendeleo ya nchi yetu tayari serikali imeamua kutoa hadhi maalum kwa Diaspora na hivi sasa serikali inakamilisha taratibu za kuwapa hadhi maalum na muda si mrefu Diaspora watapatiwa hadhi maalum."

Katika swali la msingi, mbunge huyo alihoji Tanzania ina Diaspora wangapi na ni upi mchango wao katika uchumi wa nchi.

Akijibu swali hilo, Naibu Waziri huyo alisema kwa mujibu wa taarifa kutoka Ofisi za Uwakilishi wa Kibalozi na maeneo yake ya Uwakilishi, idadi ya Diaspora wa Tanzania ni Milioni 1.5 na kwamba mfumo huo utasaidia ukusanyaji endelevu wa takwimu za Diaspora.

"Diaspora huchangia katika maendeleo ya nchi kwa kutuma fedha za kigeni nchini (Remittances), kuwekeza, kuleta mitaji, utaalamu na Teknolojia inayoweza kuchangia kukuza uzalishaji wa mazao, bidhaa na huduma mbalimbali zenye tija kiuchumi," alisema.

Aidha, alisema Diaspora hutangaza fursa za kiuchumi, biashara, utalii na uwekezaji zinazopatikana nchini.

"Mathalan katika kipindi cha kuanzia mwezi Januari hadi Desemba 2022, Diaspora wa Tanzania walituma nchini kiasi cha Dola za Marekani Bilioni 1.1 sawa na Sh. trilioni 2.6," alisema.

Opia alisema alisema katika kipindi hicho, Diaspora walifanya uwekezaji kupitia ununuzi wa nyumba na viwanja wenye thamani ya Sh.Bilioni 4.4 na ununuzi wa hisa zenye thamani ya Sh. bilioni 2.5.

# SUA yaandaa wiki kumuenzi Sokoine kwa utendaji kazi, uzalendo kwa taifa

**Na Christina Haule,** MOROGORO

MCHANGO wa aliyekuwa Waziri Mkuu, Hayati Edward Moringe Sokoine, unaendelea kukumbukwa na kutumiwa katika Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo (SUA) kwa sababu ya ushupavu, uzalendo na uchapakazi aliouonesha katika taifa la Tanzania.

Kaimu Makamu Mkuu wa SUA, Prof. Amandus Muhairwa, alisema juzi kuwa kumbukizi ya 18 ya Sokoine kwa vipindi viwili kuanzia mwaka 1977 hadi 1980 na mwaka 1983 hadi 1984, itafanyika rasmi kuanzia Mei 23 hadi 26, mwaka huu, kwa sababu ya kuenzi historia yake iliyofungamanishwa na historia ya kuanzishwa kwa chuo hicho.

Prof. Muhairwa alisema pamoja na elimu wanayoitoa kuanzia ukaribisho wa wanafunzi mwaka wa kwanza, wanawajenga wanafunzi kupitia mafunzo na kazi wanazofanya juu ya masuala ya uchapakazi kwa vitendo. Katika kufanya hivyo, alisema wanatarajia mwanafunzi akitoka hapo awe na ujasiri na uchapakazi na hawatarajii mwanafunzi apate digrii kiulaini.

"Mwanafunzi yeyote aliyepo SUA anayepata digrii anaipata kwa uchapakazi na anakuwa amefanya kazi kwa juhudi kubwa sana na maarifa na ndio sifa kubwa sana ya uchapakazi aliyokuwa nayo Sokoine. Kingine ni ubunifu sababu Sokoine alikuja na mawazo mbalimbali ya kurekebisha nchi kitu ambacho kilikuwa kigumu sana. Aliweka sawa ubunifu ambao nao tunawaelimisha wanafunzi kuwa wabunifu wazuri. Pia uadilifu ambao nasi tunapambana wakati wote kuwafanya wanafunzi na taasisi yote kuwa waadilifu.

Jambo linguine ni ufuatiliaji ambao alikuwa anautumia sana hata kufikia wakati kuweka mijadala juu ya nchi kukosa chakula mwaka 1980 pia tunawafundisha wanafunzi uhalisia pia ambao aliutumia sana nasi tunautumia kuelimisha. Na hapo itamfanya mwanafunzi kwenda kumsaidia hata mama yake aliyeko kijijini sana ambaye ana elimu ya chini kabisa na kumfikisha katika hali ambayo itamnyanyua na kuwa na maisha bora," alisema.

Mkuu huyo pia alisema Sokoine alisimamia kupitishwa muswada wa sheria ya kuanzisha Chuo Kikuu cha Kilimo cha Morogoro na kwamba baada ya kifo chake na kwa heshima yake, jina la chuo lilibadilishwa na kuwa Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo (SUA) kuanzia Julai Mosi, 1984.

Alisema uamuzi wa kupitisha kumuenzi Hayati Edward Sokoine ulifanywa na Seneti ya SUA kwa kufanya maadhimisho kila mwaka ambayo yalianza kufanyika tangu mwaka 1992.

Prof. Muhairwa alisema kiongozi huyo shupavu alikuwa mwenye msimamo wa kipekee katika historia ya viongozi wa ngazi za juu Tanzania.

Alisema Sokoine alikuwa mzalendo na mwenye mawazo yenye fikra na mwelekeo wake juu ya suala la maendeleo na alihakikisha yanathibitika katika aliyoyasimamia bila woga ikiwa ni pamoja na kujitegemea na uhuru wa kitaifa sambamba na kujitosheleza kwa chakula, soko la kitaifa na maendeleo vijijini.

Wiki ya Kumbukizi ya Sokoine kwa mwaka huu ina kaulimbiu isemayo "Mazingira Wezeshi kwa Vijana Kushiriki Katika Kilimo: Sera, Miongozo na Utendaji" ambayo inaandaa fursa kwa vijana katika sekta ya kilimo.

Naye Mwenyekiti wa Kamati ya Maandalizi ya Kumbukizi hiyo, Prof. Samuel Kabote, alisema duniani kote vyuo huanzishwa kwa lengo la kutoa mafunzo, utafiti na mambo mbalimbali lakini SUA ilianzishwa na kujikita zaidi katika mambo hayo na mafunzo kwa vitendo ili mtu anayezalishwa hapo awe mtendaji anayeweza kutenda jambo likaonekana kitu ambacho kinafungamanisha na Sokoine mwenyewe na kuwa tofauti na vyuo vingine.

# Dar kuendesha operesheni mifuko ya plastiki

**Na Joseph Mwendapole**

MKUU wa Mkoa wa Dar es Salaam, Amos Makala, amesema wanatarajia kuendesha operesheni ya kuwasaka wazalishaji na wasambazaji wa mifuko ya plastiki inayotumika kama vifungashio ambayo imepigwa marufuku.

Juni Mosi 2019, serikali ilitoa katazo la matumizi ya mifuko hiyo na utekelezaji wake ulifanikiwa kwa kiwango kikubwa ingawa katika siku za hivi karibuni, mifuko hiyo imerejea upya na imejaa kwenye masoko mbalimbali nchini.

Makala aliyasema hayo jana wakati wa mkutano ulioandaliwa na Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC) kwa watendaji wote wa halmashauri za mkoa wa Dar es Salaam.

Mkutano huo pia uliwashirikisha wamiliki wa kumbi za starehe, baa, wakuu wa masoko, wazalishaji na watumiaji wa mifuko ya plastiki ambayo inatumika kama vifungashio vya bidhaa mbalimbali nchini.

Makala aliipongeza NEMC kwa kuandaa mkutano huo ambao aliuelezea kuwa ni muhimu kwa kuwa umewashirikisha watendaji wa ngazi mbalimbali kwenye halmashauri ambao wako karibu na masoko.

"Mliponishirikisha nilikubali haraka kwa sababu ni sehemu ya kazi yangu na mimi na NEMC tumefanyakazi nyingi sana katika kukabiliana na hii mifuko. Kwa hiyo ninatarajia kikao hiki kitatuletea mabadiliko makubwa kwenye mkoa wetu," alisema.

"Tulianza kukutana na viongozi wa dini Kijitonyama mwaka jana nikateta nao kuhusu athari za kelele za mitetemo na kuna mambo ya msingi tulikubaliana tulikotoka, tulipo na tunakokwenda. Tulipokea changamoto mbalimbali ambazo kwa kiasi kikubwa zinachangiwa na watendaji wa mitaa na kata wa halmashauri kwa kutoa vibali holela," alisema. Mkuu wa mkoa alisema kuna maeneo maalum ambayo yametengwa kwa ajili ya makazi lakini baadhi ya watendaji wamekuwa wakibadilisha matumizi na kutoa vibali vya watu kufanya biashara na kujenga nyumba za ibada hali ambayo imekuwa ikisababisha malalamiko kutoka kwa wananchi wanaoishi jirani na maeneo hayo.

"Nashukuru Mkurugenzi Mkuu wa NEMC ametenga siku nyingine ya kukutana na viongozi wa dini kujadili tunayojadili leo. Sasa kelele mitaani imekuwa changamoto sana napata jumbe nyingi sana watu wengine wananitumia sauti wanasema huo mziki unapigwa jirani yangu wanasema serikali iko wapi sisi huku hatulali," alisema.

Kwa mujibu wa Makala, wamiliki wa baa na kumbi za starehe wamefannya uwekezaji lakini lazima wafuate sheria na kanuni zilizowekwa kwa kuhakikisha kiwango cha kelele na mitetemo wanachotoa kimethibitishwa na NEMC.

"Raha usijipe wewe tu na ukapeleka kero kwa watu wengine. Kwa mfano jirani yako ana makazi na familia, wewe unafurahia kupata pesa na wateja wako lakini unasababisha usumbufu mkubwa kwa majirani, ndiyo sababu kuna kiwango cha mtetemo kinachokubalika kwa mujibu wa sheria. Sasa NEMC au maofisa mazingira wakija kukufungia unaanza kutafuta huruma mitandaoni.

"Ukienda Feri, Coco Beach na hata kwa wauaza samaki wanawawekea chachandu wateja wao kwenye mifuko iliyopigwa marufuku, buchani wanakata nyama na kuweka kwenye vifungashio vilivyopigwa marufuku. Hii haikubaliki na hatuwezi kuiacha hali hii iendelee," alisema.

Mkurugenzi Mkuu wa NEMC, Dk. Samuel Gwamaka, alisema baraza limekuwa linapokea malalamiko mengi ya kelele kwenye baa na kumbi za starehe kutoka kwenye maeneo mbalimbali.



Diwani wa Kata ya Kivukoni, Sharik Choughule (mbele), akikagua ukarabati wa baadhi ya majengo ya Shule ya Msingi Bunge, jijini Dar es Salaam mapema wiki hii. Wengine ni watendaji wa kata hiyo. **PICHA: MPIGAPICHA WETU.**

# Ofisa NHC kortini madai ya rushwa

**Na Grace Gurisha**

OFISA Milki wa Shirika la Nyumba la Taifa (NHC), Fadhili Kasegese ,amepandishwa kizimbani katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu, Dar es Salaam akikabiliwa na mashtaka kushawishi na kupokea rushwa Sh. milioni tatu.

Akisoma hati ya mashitaka jana mbele ya Hakimu Mkazi Mkuu Ramadhani Rugemarila, Wakili wa Serikali kutoka Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU), Mwanakombo Rajabu, alidai kuwa mshtakiwa anadaiwa kuomba na kupokea rushwa.

Rajabu alidai kuwa Machi 27, mwaka huu, mshtakiwa akiwa kama ofisa milki wa NHC Mkoa wa Ilala, alishawishi rushwa ya Sh. milioni nne kutoka kwa Vishal Dharsi.

Ilidaiwa kuwa alishawishi rushwa hiyo kutoka kwa Dharsi ili asimtoe katika nyumba iliyoko kitalu namba moja iliyoko eneo la Msimbazi, Ilala jijini Dar es Salaam, kitendo ambacho ni kinyume cha maagizo ya mwajiri wake.

Katika shitaka la pili, ilidaiwa kuwa Aprili 6, 2023 katika Ofisi za NHC Ilala, mshtakiwa alipokea rushwa ya Sh. milioni tatu kutoka kwa Dharsi kama kishawishi asimtoe katika nyumba hiyo.

Baada ya kusomewa mashitaka hayo, mshtakiwa alikana kuhusika na tuhuma hizo. Upande wa mashtaka ulidai kuwa upelelezi wa kesi hiyo umekamilika na kuomba tarehe nyingine ya kumsomea mshtakiwa hoja za awali.

Mshtakiwa huyo aliachiwa kwa dhamana baada ya kutimiza masharti ikiwamo kutia saini bondi ya Sh. milioni tano pamoja na kuwa na wadhamini wawili wenye vitambulisho ambao pia walitia saini bondi ya kiasi hicho cha fedha.

# Serikali yashauriwa kutoa mafunzo ya kupunguza ukatili kwa watoto

**Na Beatrice Shayo**

SERIKALI imeshauriwa kutoa mafunzo ya malezi kwa wazazi na walezi ili kupunguza vitendo vya ukatili kwa watoto vinavyofanyika nyumbani na kuepusha watoto kukimbilia mtaani.

Ushauri huo ulitolewa juzi jijini Dar es Salaam na Meneja wa Shirika la Railway Children (RCA), Rose Kagoro, wakati akizungumza na waandishi wa habari kuhusu kuadhimisha siku ya mtoto anayeishi na kufanya kazi mtaani ambayo hufanyika Aprili 12 kila mwaka.

Alisema kuna haja ya serikali kuendelea kutoa elimu kwa wazazi lengo ni kukomesha vitendo vya ukatili kwa kuwa wameeleza wanakutakana na vitendo hivyo hali inayosababisha kukimbia nyumbani.

Kagoro alisema kama jitihada madhubuti na za makusudi hazitachukuliwa watoto hao wataendelea kuteseka kwa kukosa haki zao na hivyo kuendelea kutengeneza kizazi cha watoto wanaoishi na kufanya kazi mtaani.

"Serikali kwa kushirikiana na wadau kubuni na kutekeleza mikakati mbalimbali ya kudhibiti wimbi la watoto wanaotoroka familia zao na kukimbilia mitaani ikiwamo kufanyia kazi changamoto zinazokabili watoto katika familia zao," alisema Kagoro.

Aidha, alisema Shirika lake linaungana na wadau mbalimbali duniani kuadhimisha siku hiyo kwa kukumbusha umuhimu wa kuhakikisha jitihada za kuwaunganisha watoto wanaoishi na kufanya kazi mtaani na familia zao zinazingatia usalama wa watoto kwa kipindi chote wanachokuwa mtaani.

Alisema wanaipongeza serikali kwa juhudi wanazozifanya katika kuboresha ulinzi, usalama na ustawi wa watoto walio katika mazingira hatarishi ikiwamo watoto wanaoishi na kufanya kazi mtaani.

Kagoro alisema katika kuunga mkono jitihada mbalimbali zinazofanywa na serikali, RCA imeendelea kuhudumia kundi hilo la watoto ikiwamo kuwaunganisha na familia zao.

Alisema katika kipindi cha mwaka jana wameunganisha watoto 303 na familia zao, 337 kurudi shule, mafunzo ya stadi za maisha kwa vijana 94 na wazazi na walezi 217 walipatiwa mafunzo ya malezi chanya.

Ofisa Ulinzi na Usalama kwa Mtoto kutoka RCA, Mary Mushi, alisema kuwapo kwa watoto wa mitaani moja wapo ya sababu waliyoeleza inayotokana na migogoro ya familia na hali duni ya maisha.

Alisema mipango yao ni kuzuia watoto kufanya kazi mitaani ili kutokomeza suala hilo inahitajika ushirikiana baina ya serikali, wadau, wananchi na jamii kuondoa ukatili unaofanywa katika kaya ambavyo ni sababu ya watoto kuingia maisha ya mitaani.

# MAONI & UCHAMBUZI

Nipashe
MWANGA WA JAMII

## Simba, Yanga onyesheni ukubwa, ukongwe kesho

**SIMBA** na Yanga zote kutoka Kariakoo, zinatarajia kukutana katika mechi ya marudiano ya Ligi Kuu Tanzania Bara msimu huu itakayochezwa kesho kuanzia saa 11:00 jioni kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam.

Vigogo hao wa soka nchini wanakutana wakiwa na kumbukumbu ya kutoka sare ya bao 1-1, katika mechi ya kwanza iliyochezwa Oktoba, mwaka jana, Pape Sakho akifunga kwa upande wa Simba na Stephane Aziz Ki, akiisawazishia timu yake ya Yanga.

Simba ambao ni wenyeji wa mechi hiyo wao watashuka dimbani wakiwa na kumbukumbu ya ushindi wa mabao 2-0 walioupata dhidi ya Ihefu SC ya Mbarali, Mbeya, timu iliyokatisha unbeaten za Yanga wakati mabingwa hao watetezi na vinara wa Ligi Kuu Tanzania Bara wao waliichapa bila huruma Kagera Sugar magoli 5-0.

Mechi ya kesho mbali na kuendeleza ubabe, ni mchezo utakaotoa picha na mwelekeo wa mbio za ubingwa wa ligi hiyo inayoelekea ukingoni, Yanga ikishinda itakuwa imezidi kulikaribia taji hilo wakati Simba itakuwa imejiimarisha kwenye vita hiyo na kuamini lolote linaweza kutokea katika mechi zilizobakia.

Wekundu wa Msimbazi wako nyuma kwa pointi nane, ikiwa imebakia michezo minne kwa kila timu, kama ambavyo hakuna timu yenye uhakika wa kushuka daraja ingawa Polisi Tanzania wanaoburuza mkia wanahitaji kufanya miujiza, ndivyo ilivyo kwa ushindani kwa walio juu kwenye msimamo wa ligi hiyo.

Ukiondoa vita ya ubingwa, mashabiki na wanachama wa timu hizo kongwe wanahitaji kuona burudani na soka la kiwango cha juu kutoka kwa wachezaji wao ambao msimu huu wameonyesha kupambana zaidi kwenye michezo ya kimataifa ya Ligi ya Mabingwa Afrika na Kombe la Shirikisho Afrika.

Ili kuonyesha ukubwa, nyota wa Simba na Yanga kesho mnatakiwa kuonyesha darasa kwa wachezaji chipukizi kwa kucheza kwa nidhamu, bidii na kutumia maarifa kwa sababu ya kutaka kusaidia kupata ushindi na hatimaye kufikia malengo.

Mchezaji mwenye uzoefu huonekana na hupimwa kupitia mechi kubwa, huu ni wakati mwingine muhimu kwa wachezaji wa Simba na Yanga kupambana na kuonyesha thamani yao.

Wachezaji wanatakiwa kufahamu kupitia mechi hiyo, wanaweza pia kujifungulia milango ya mafanikio ya kimataifa kwa sababu mawakala, makocha na wadau mbalimbali wanatarajia kuufuatilia mchezo huo kupitia njia mbalimbali, Simba na Yanga ni moja ya dabi kubwa barani Afrika.

Kiwango bora na kutekeleza majukumu vyema, ni vitu vikubwa vitakavyosaidia timu kupata matokeo chanya, ingawa pia kuna wale wanaoamini bahati huwa na nafasi yake katika mechi hii.

Hesabu nzuri za makocha katika kupanga kikosi ni jambo linalotegemewa, lakini pia matokeo mazuri huendelea kuwapa walimu nafasi ya kujitangaza na kuongeza thamani yao.

Hata hivyo wachezaji, benchi la ufundi na viongozi wa pande zote mbili mnatakiwa kutumia mechi ya kesho kuwajenga wachezaji wenu kuelekea michezo ya hatua ya robo fainali ya mashindano ya CAF, kwa kujiimarisha na kutumia mechi hiyo vizuri, kutasaidia kuwaongezea hali ya kujiamini.

Kiufundi mchezo huu utasaidia kupata matokeo chanya kuelekea hatua ya robo fainali ambayo Simba itakutana na Wydad Casablanca wakati Yanga itaanza kwa kuwafuata Rivers United huko Nigeria.

Tunawakumbusha wachezaji na wadau wote wanaohusika kuhamishia nguvu za maandalizi ya mechi hii ya watani wa jadi kwenda katika michezo miwili ya robo fainali, kwa kufanya hivyo, Tanzania inaweza kuweka rekodi nyingine nzuri ya kuingiza timu mbili kwenye hatua ya nusu fainali.

Bila kusahau mashabiki nao wanatakiwa kufahamu mipaka yao huku waamuzi wakitakiwa kuchezesha kwa kufuata kanuni 17 za mchezo huo wenye mashabiki wengi duniani.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:

**THE GUARDIAN LIMITED**

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677-020701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






Na Adam Fungamwango

# Muungwana Lazima Nilonge

## Waamuzi watende haki dabi, mashabiki watulie

**KESHO** ni siku ambayo mashabiki wa soka Tanzania, Afrika Mashariki na Kati itashuhudia mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara kati ya watani wa jadi, Simba na Yanga.

Ni mechi ya mzunguko wa pili baada ya ile ya kwanza iliyochezwa Oktoba 23, mwaka jana kumalizika kwa sare ya bao 1-1.

Siku zote, mechi hii inavuta hisia za mashabiki wengi hata hapa nchini ambao wanaufutiliwa kwa kuutazama uwanjani, maeneo mbalimbali kwenye luninga ikiwamo vibanda umiza, hata wale watakaokuwa wakisikiliza katika redio, majumbani au kwenye vyombo vya usafiri.

Tumewasikia makocha wote wakisema wamejiandaa kikamilifu na pambano hilo. Makocha, Juma Mgunda na Cedric Kaze kila mmoja akitamba kwa wachezaji wao wako tayari na wanachosubiri ni kipenga cha mwamuzi tu.

Hapa tunaona tayari makocha hao na wakuu wao wameshakamilisha kazi yao, wanachosubiri ni wachezaji kufanya kile ambacho wametumwa na walimu wao.

Binafsi ninatarajia itakuwa moja ya pambano bora kwa sababu si mara nyingi kuziona timu hizo mbili zikienda kupambana zikiwa bora.

Mara kwa mara kama Simba ni bora, basi Yanga itakuwa ya kuungaunga, na kama Yanga itakuwa iko vizuri, Simba itakuwa tia maji tia maji.

Hata hivyo hilo mara zote haliondoi mshindi anakuwa hatabiriki kwa sababu Simba na Yanga zote zimeshawahi kushinda 'dabi' mmoja akiwa si bora kuliko mwenzake.

Kwa sasabu safari hii timu zote zina wachezaji bora na wanajiamini, naamini wachezaji wataweka mpira chini na kucheza kwa kupambana, kujituma na kwa kiwango cha juu, lakini si kukamiana na kuumizana.

Kuna wakati baadhi ya wachezaji wanadhani mechi za Simba na Yanga ni za kucheza rafu zisizo za msingi na wanafanya hivyo kwa makusudi kwa sababu wanajua waamuzi kwenye pambano hili kwa miaka ya hivi karibuni wamekuwa waoga kutoa kadi inapobidi kufanya hivyo.

Wachezaji wa Simba na Yanga wakumbuke wote baada ya hapo wana vibarua vya kwenda kuiwakilisha nchi na klabu zao kwenye mechi za kimataifa, hivyo kuchezeana mchezo ambao si wa kiungwana na kuumizana, ni kuukosea heshima au kuuhujumu mpira wa Tanzania.

Kama nchi kwa sasa imekuwa ikizisapoti timu hizi ambazo zote zimetinga hatua ya robo fainali ya michuano hiyo, hivyo kitendo cha mchezaji yoyote kufanya rafu za makusudi ni kama kuhujumu soka la Tanzania lisisonge mbele.

Kinachotakiwa kila mmoja acheze kwa uwezo wake, apambane kunyang'anya mpira na rafu zile ya kiufundi ambazo zipo kwenye soka, lakini si za kuumizana eti kwa sababu tu ni 'dabi'.

Upande wa waamuzi nao wawe makini na hilo. Kwanza kabisa watende haki kama inavyotakiwa bila ya kuegemea upande wowote.

Lakini wanapaswa kuwa wakali kwa sababu wachezaji wa timu hizi kutokana na timu zao ni kubwa, wanakuwa wababe hata kwa mwamuzi, wakiamini hawawezi kufanywa lolote.

Waamuzi wasiruhusu mchezaji yoyote kuwatia vidole vya macho halafu wakafumbia macho, lakini pia wasiache rafu za kijinga zikatawala kwani huko mbele watashindwa kudhibiti wengine watakaporudishia.

Yoyote atakayeanza kufanya hivyo anatakiwa aonywe vikali ili kuwakumbusha wengine kuwa mwamuzi yupo, mkali na ni makini.

Mashabiki wanataka baada ya mechi wazungumziwe wachezaji. Wazungumzie ubora wa wachezaji jinsi walivyoonyesha viwango vya kwenye 'dabi' ile na si nyota wa mchezo awe waamuzi. Yaani wao ndiyo wazungumziwe zaidi kuliko wachezaji.

Mwisho ni kwa mashabiki uwanjani, wanatakiwa wasiende na matokeo kwa sababu mechi hiyo haitabiriki.

Kuna makosa ya kibinadamu ya waamuzi ambayo dunia nzima yapo. Yasiwe ndiyo chanzo cha kuwaponda na kuwalamu waamuzi wakiona kuwa wao ndiyo wamesababisha kufungwa na kupoteza mechi.

Baadhi ya mashabiki wana nongwa. Kuna baadhi ya makosa ya waamuzi ni ya kawaida na hayaathiri matokeo au mchezo, lakini wao wataona ndiyo yaliyosababisha wafungwe. Waache mihemko. Nawatakiwa mchezo mwema.

## HABARI KITAIFA

# TANESCO: Mvua haitoshelezi kwa umeme

**Na Maulid Mmbaga**

SHIRIKA la Umeme Tanzania (TANESCO) limesema mvua zinazoendelea kunyesha bado hazijasaidia kutoa kiwango cha juu cha maji kitakachowezesha kupatikana kwa umeme wa uhakika.

Taarifa iliyotolewa jana na Msemaji wa Shirika hilo, Elihuruma Ngowi, ilisema wamekagua mabwawa ya kufua umeme kwa njia ya maji kikiwamo kituo cha Hale, ambacho kinazalisha megawati 21 na kwamba kwa sasa kutokana na mtiririko wa maji kinazalisha wastani wa megawati 10.5.

Alisema kituo kingine ni New Pangani Falls ambacho kina uwezo wa kuzalisha megawati 68 na kwamba uwezo wake umepungua kutokana na mtiririko mdogo wa maji na kwa sasa kinazalisha megawati 10 asubuhi na 40 jioni.

"Pia tulifika kwenye kituo cha Kidatu ambacho kina uwezo wa kuzalisha megawati 204 lakini kutokana na mtiririko wa maji, mitambo iliyoko inafua umeme wa megawati 194.

"Bwawa lingine ambalo tumejionea ni Mtera lililoko mkoa wa Dodoma ambalo lina uwezo wa kuzalisha megawati 80. Lakini kutokana na mtiririko wa maji kuwa wa wastani, umeme unaozalishwa kwa sasa ni megawati 75, hali inayosababisha kuwe na upungufu wa megawati tisa," alisema Ngowi.

Aliongeza kuwa pamoja na mvua kunyesha kwa ujumla kitu ambacho wamekioni ni kwamba bado hazijawawezesha kupata maji ya kutosha katika vyanzo vyao vya kuzalishia umeme.

Mtaalamu wa mabwawa ya kufua umeme, Simon Lauwo, alisema TANESCO si mara ya kwanza kukutana na hali hiyo lakini wameweka mipango mizuri ya kuhakikisha kwamba vyanzo walivyonavyo vinatumika kwa wakati mmoja.

"Tumeweka mikakati ya kuhakikisha vyanzo vyetu vinatumika kwa wakati mmoja vikisaidiana ili kuhakikisha kwamba umeme wa uhakika unapatikana kwa wananchi na shughuli za kiuchumi zinaendelea kufanyika bila kusimama.

Hata hivyo, shirika bado tuna imani kubwa kuwa umeme utakapatikana wa kutosha na tunaomba Mungu kwamba hali iendelee kuwa nzuri ili tuendelee kuzalisha umeme kukidhi mahitaji ya Watanzania," alisema Lauwo.



Mkuu wa Mauzo wa Vodacom Tanzania mikoa ya Dar es Salaam na Pwani, Brigita Shirima akizungumza wakati wa uzinduzi wa kampeni mpya ya 'Zaidi ya Mtandao' kwa wateja katika soko la Mabibo jijini Dar es Salaam jana, itakayowawezesha wateja wapya kutuma na kutoa pesa bila ya tozo kwa miamala chini ya 50,000/- kupitia M-Pesa. **PICHA: MPIGAPICHA WETU.**

# DART kupanda miti 1,000 Dar es Salaam

**Na Joseph Mwendapole**

WAKALA wa Mabasi Yaendayo Haraka (DART), imepanga kupanda miti zaidi ya 1,000 kwenye kilomita 154, maeneo ya jijini Dar es Salaam ambayo mabasi hayo yanapita.

Mkurugenzi wa DART, Dk. Edwin Mhede, alisema hayo wakati wa uzinduzi wa upandaji wa miti hiyo kwenye kituo cha mabasi hayo, Ubungo.

Hafla hiyo pia ilihudhuriwa na Mkuu wa Wilaya ya Ubungo, Hashim Komba na viongozi mbalimbali wa Mkoa wa Dar es Salaam wakiwamo wa benki ya NMB.

Dk. Mhede alisema kabla ya ujenzi wa miundombinu hiyo kulikuwa na uoto wa asili na miti ya aina mbalimbali na DART inawajibika kuirejesha hali hiyo.

"Sisi tunapojenga barabara kwa kiasi kikubwa tunaharibu uoto wa asili na miti kwa sababu kama kulikuwa na mti tunaukata na nyinyi mliokuwa Dar es Salaam wakati huo naamini mnakumbuka hali ilivyokuwa hapa Ubungo kabla ya ujenzi huu, ile hali haipo tena ndiyo sababu tunaona tunawajibika kuirejesha," alisema Dk. Mhede.

Alisema asilimia 45 ya wakazi wa Dar es Salaam wanatumia njia za kwenda kwa miguu (shoroba), ambazo kwa sasa hazina miti ambayo zamani iliwasaidia kupita kivulini hali ambayo alisema lazima irejee.

Mkuu wa Wilaya ya Ubungo, Hashim Komba, alisema uzinduzi wa upandaji miti hiyo ni jambo kubwa na la kihistoria kwa wakazi wa Ubungo kwa kuwa itasaidia kwa kiwango kikubwa kurejesha mazingira yaliyoharibiwa kutokana na shughuli mbalimbali za ujenzi.

"Mazingira ni uhai hivyo ukiyahifadhi mazingira na yenyewe yatakuhifadhi ukiyaharibu na yenyewe yatakuadhibu kwa hiyo natoa wito kwa wananchi wa Ubungo waunge mkono kampeni hii kwa kutunza miti itakayopandwa, kila mtu ambaye miti hii itapandwa mbele ya nyumba yake au eneo lake la biashara atawajibika kuitunza," alisema.

Alisema alishatoa maelekezo kwa viongozi wa mitaa na kata kuitambua miti hiyo na kuitunza kwa hali na mali itakapopandwa na DART na wafanyabiashara ndogo ndogo wafanye sehemu ambazo hazina miti.

Aliwataka Watanzania kuona fahari ya kupanda miti kwa kushiriki vyema kwenye kampeni ya upandaji miti kwa mkoa mzima akisema kuwa hata yeye binafsi amekabidhiwa mti ambao ameupanda na kuuwekea alama kwa ajili ya kuhakikisha anafuatilia ukuaji wake.

Alisema viongozi wa kitaifa, Rais Samia Suluhu Hassan, Makamu wa Rais, Dk. Phillip Mpango na Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, wamekuwa mstari wa mbele kuhamasisha upandaji wa miti kwa ajili ya kuhifadhi mazingira na wananchi wanapaswa kuiga mfano huo kwa kupanda miti.

## Serikali kushughulikia ustawi sekta uchukuzi

**Na Mary Geofrey**

SERIKALI imeihakikishia sekta binafsi itayafanyia kazi matatizo yote yanayokwamisha ustawi wa maendeleo ya sekta ya uchukuzi nchini.

Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, Prof. Makame Mbarawa, aliyasema hao juzi Dar es Salaam, kwenye mkutano wa majadiliano ya kisekta ya wizara na wadau wa sekta binafsi.

Alisema mkutano huo ambao ni utekelezaji wa agizo la Rais Samia Suluhu Hassan, una lenga kushughulikia changamoto zote kwa wakati.

"Serikali itaendelea kuboresha mazingira mazuri ya kufanya biashara kwa sekta ya usafirishaji na usafiri sambamba na kuzifanyia kazi sheria na kanuni mbalimbali ambazo hazikidhi matarajio ya ukuaji wa sekta hii," alisema Prof. Mbarawa.

Aliahidi kufanyia kazi suala la udhibiti mwendo kwa kuielekeza Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini (LATRA), kulifanyia kazi kwa kushirikiana na Shirika la Viwango Tanzania (TBS).

Prof. Mbarawa aliwaeleza wadau kuwa serikali itaendelea kuimarisha miundombinu ikiwamo ujenzi wa njia nne kutoka Bandari ya Dar es Salaam, Barabara ya Morogoro, Mbeya hadi Tunduma.

Katibu Mtendaji wa Baraza la Taifa la Biashara (TNBC), Dk. Goodluck Wanga, aliwapongeza wadau kuwa wazi na kueleza matatizo yanayowakabili.

"Mikutano hii ya kisekta ni muhimu kwani inasaidia serikali kutafuta suluhisho la kudumu kwa changamoto, vilevile kuimarisha mazingira ya kufanya biashara".


**KUPOTEA KWA KADI YA GARI**

HUATENG METALLURGICAL CO. LTD anatangaza kupotea kwa kadi ya gari aina ya NISSAN XTRAIL yenye usajili namba: T186 DGQ , CHASSIS NAMBA: NT30135365 na ENGINE NAMBA: QR20515987A. kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. POLISI TAARIFA: DAR/URA/RB/118025/2023

HABARI KITAIFA

# Mgodi watoa msaada kituo cha afya

**Na Mwandishi Wetu,** TARIME

MGODI wa Dhahabu wa Barrick North Mara na makandarasi wake wamekabidhi msaada wa vifaa tiba vyenye thamani ya Sh. milioni 120 katika Kituo cha Afya Sungusungu kilichoko Nyamongo, Tarime mkoani Mara.

Hafla ilifanyika katika kituo hicho na kuhudhuriwa na wafanyakazi wa mgodi, wawakilishi kutoka kampuni zinazofanya kazi katika mgodi, viongozi wa serikali wilayani Tarime na Mbunge wa Tarime Vijijini, Mwita Waitara.

Akikabidhi msaada huo, Meneja Mkuu wa North Mara, Apolinary Lyambiko, alisema kampuni imeshirikiana na Makandarasi kuchanga dola za Marekani 59,587.60 kwa ajili ya ununuzi na ufungaji wa vifaa hivyo.

"Desemba, mwaka jana, mimi na wafanyakazi wenzangu tulitembelea kituo hiki na kujionea mapungufu ya vifaa tiba. Kwa kuzingatia umuhimu wa kituo hiki katika utoaji wa huduma za afya kwa wananchi na wafanyakazi wa mgodi, Januari 2023 niliagiza idara yetu ya uhusiano na ile ya Afya kuandaa kikao na Makandarasi wanaofanya kazi mgodini ili kwa pamoja tuone namna tunavyoweza kuchangia ununuzi wa vifaa tiba," alisema Lyambiko.

Alisema vifaa hivyo vilivyokabidhiwa vitasaidia kuwezesha upatikanaji wa huduma bora za afya zikiwamo za mama na mtoto katika kituo hicho na kwamba msaada huo ni sehemu ya uwajibikaji wa mgodi na makandarasi kwa jamii inayouzunguka.

"Malengo ya mgodi ni kuendelea kushirikiana na makandarasi wote kama wadau muhimu katika kutekeleza shughuli mbalimbali za uwajibikaji kwa jamii inayotuzunguka ili kuimarisha uhusiano na mshikamano," alisema Lyambiko.

Baadhi ya kampuni za makandarasi zilizoshirikiana na mgodi kufanikisha msaada huo ni Kemanyanki, RES, Wings, Boart Longyear, AKO na PKM.

Akipokea na kukabidhi vifaa tiba hivyo kwa uongozi wa Kituo cha Afya Sungusungu na Halmashauri ya Wilaya ya Tarime, Waitara aliushukuru mgodi huo na makandarasi hao, akisema wameweka alama nzuri katika eneo hilo.

"Haya yote ni matunda ya mahusiano na ushirikishwaji," amesema Mbunge Waitara na kuahidi kuandika barua ya kuushukuru mgodi na makandarasi hao kutokana na msaada huo wa vifaa tiba.

Kaimu Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Tarime, Sylvanus Gwiboha, alishukuru na kusema msaada huo una maana kubwa katika utoaji wa huduma bora za afya.




Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Tarime, mkoani Mara, Simion Kiles Samwel (kushoto), akizungmza na viongozi wa Kamati za Maendeleo ya jamii, wakati wa mafunzo ya siku tatu ya kuibua na kusimamia utekelezaji wa miradi ya kijamii na kiuchumi yanayoendeshwa na wataalamu kutoka Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kwa ufadhili wa kampuni ya Barrick, wilayani humo juzi. Wengine ni Mbunge wa Tarime Vijijini, Mwita Waitara (wa tatu kulia) na viongozi wa halmashauri hiyo. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Benki yaahidi kuwekeza katika ubunifu

**Na Mwandishi Wetu**

BENKI ya BancABC Tanzania, ambayo ni kampuni tanzu ya Atlas Mara imesema itaendelea kuwekeza kwenye bidhaa na huduma bunifu ili kuendana na hali halisi ya maisha ya wateja wake.

Mkurugenzi Mtendaji wa BancABC Tanzania, Imani John, alisema hivi karibuni wakati wa futari iliyoandaliwa na benki hiyo kwa wateja wake.

BancABC Tanzania iliandaa futari hiyo ambayo ilileta zaidi ya watu 300 na kuongozwa na Kaimu Shekhe wa Mkoa wa Dar es Salaam, Walid Al-hadi Omar, ambaye alitoa wito kwa Watanzania wote bila ya kujali dini zao kuonyesha umoja na mshikamano wakati huu wa mwezi Mtukufu wa Ramadhan.

Tumeandaa futari hii ili kuonyesha Umoja na vile tunavyowajali wateja wetu, alisema Iman huku akisema kuwa benki hiyo imekuwa na utamaduni wa muda mrefu wa kuandaa futari ikiwa ni ishara ya kuonyesha upendo kwa kipindi cha mwezi Mtukufu wa Ramadhan.

"Tumekuwa na utamanduni wa kuandaa futari kila mwaka kama ishara ya kuonyesha upendo kwa wateja wetu na uaminifu wao kwa kutuchangia sisi kama benki yao," alisema na kuongeza kuwa matukio kama hayo ni muhimu kwa kuwa pia ni muda mwafaka wa kuzungumza na wateja na kujua mahitaji yao. Kuhusu bidhaa na huduma ambazo hutolewa na benki hiyo, alisema: "Sisi BancABC tumekuwa tukitoa huduma na bidhaa ambazo zinagusa Watanzania wa kada zote kama vile wateja binafsi, wajasiriamali wadogo na wakubwa pamoja na wateja wakubwa ambazo ni huduma za kuweka na kutoa fedha pamoja na mikopo nafuu.

"Huduma na bidhaa zetu hizi ni za ubunifu wa hali ya juu na tutaendelea kuwekeza kwenye ubunifu ili kuendana na hali halisi ya maisha ya kila Mtanzania."

Aliongeza benki imejikita kwenye huduma za kimtandao "kidijitali" ili kuwezesha Watanzania wengi walio nje na ndani ya nchi kuendelea kufanya miamala na kukuza pato la taifa. Alitaja baadhi ya huduma hizo ni Pamoja na kadi za malipo ya awali "pre-paid card" kwa sarafu tano tofauti ikiwemo TZS, USD, GBP, EUR na Yuan ya Uchina, huduma za kibenki kwa njia ya simu za mkononi yani "Mobile Banking".

Huduma zingine ni za kibenki kwa njia ya intaneti ambayo mteja anaweza kufanya muamala na kutizama salio lake akiwa nyumbani au ofisini kwake kwa usalama kabisa, malipo ya serikali kwa njia za kimtandao yaani GePG pamoja na huduma za kifedha kwa njia za mawakala.

Shekhe Omar aliipongeza BancABC Tanzania kwa kuandaa futari na kusema ni ishara ya kuonyesha upendo kwa jamii ya waislamu.

'Kuandaa futari hii sio tu kuonyesha upendo kwa wateja wenu lakini pia ni ishara ya upendo kwa jamii ya waislamu wote na vizuri kwani waislamu kwenye mwezi Mtukufu kuandaliwa futari ni ishara ya upendo na kuthaminiwa', alisema Shekhe Omar.

# TEA, Sayarisafi kuwapatia wanafunzi maji salama

**Na Mwandishi Wetu**

MAMLAKA ya Elimu Tanzania (TEA) imeingia makubaliano na kampuni ya Sayarisafi Limited kwa ajili ya kuzipatia majisafi na salama shule za msingi na sekondari na kwa mwaka huu wanatarajia kuzifikia shule 100.

Makubaliano hayo yalitiwa saini juzi baina ya Mkurugenzi wa TEA, Bahati Geuzye na Mkurugenzi wa Sayarisafi, Rehema Mbalamwezi, jijini Dar es Salaam.

Mkurugenzi wa TEA, Geuzye, alisema Mamlaka hiyo imekuwa na utaratibu wa kutekeleza miradi mbalimbali ya elimu kwa kushirikiana na wadau mbalimbali na mpaka sasa wameshafanikiwa kutekeleza miradi mingi.

Aliipongeza kampuni hiyo kwa kuunga mkono jitihada za serikali kuboresha miundombinu ya elimu ya msingi na sekondari ili kuhakikisha elimu inayotolewa inakuwa bora.

Alisema kupitia TEA, wamejenga madarasa, mabweni, matundu ya vyoo, ofisi za walimu kutoa vifaa vya kujifunzia na kufundishia kwenye shule mbalimbali za msingi, sekondari na vyuo mbalimbali.

Pia, Sayarisafi Limited wanahusika na kusambaza majisafi kwenye shule mbalimbali na kupitia makubaliano hayo watafanyakazi kwa ushirikiano ili kuzifikia shule nyingi zaidi za jijini Dar es Salam na za mikoa mbalimbali.

Alitaja baadhi ya miradi waliyotekeleza kwa ushirikiano na wadau mbalimbali kuwa ni ya ujirani mwema na kwa kushirikiana na Mamlaka ya Hifadhi za Taifa (TANAPA), wamefanikiwa kujenga miundombinu ya elimu kwenye maeneo yanayozunguka hifadhi za taifa.

Mkurugenzi wa Sayarisafi Limited, Mbalamwezi, alisema kampuni hiyo inajikita katika miradi ya majisafi na salama kwenye shule za sekondari na msingi kwenye nchi mbalimbali za Afrika ikiwamo Msumbiji, Malawi na Zambia.

Alisema nia yao ni kuwawezesha wanafunzi na walimu kupata majisafi na salama ili kuwaepusha na magonjwa ya mlipuko.

"Tatizo la majisafi na salama sio la Tanzania tu ni la dunia nzima kwa sababu takribani watu bilioni 1.9 hawana uhakika wa majisafi na salama ya kunywa na watu bilioni mbili hawana vyoo kwa hiyo na sisi Watanzania tuko kwenye hiyo changamoto ambayo tunapaswa kukabiliana nayo," alisema.



## Mkoa wa Singida wapokea bil.9/- mradi wa boost

**Na Thobias Mwanakatwe,** SINGIDA

SERIKALI kwa kushirikiana na wadau imeupatia Mkoa wa Singida Sh. bilioni 9.024 kwa ajili ya kutekeleza mradi wa kuboresha upatikanaji wa fursa sawa katika ujifunzaji bora kwa elimu ya awali na msingi Tanzania Bara (boost).

Mkuu wa Mkoa wa Singida, Peter Serukamba, alisema hayo jana wakati alipokutana na wakuu wa wilaya, wakurugenzi, maofisa elimu, wahandisi na maofisa manunuzi wa halmashauri zote za mkoa huo.

Alisema fedha hizo ni maalumu kwa ajili ya ujenzi wa miundombinu ya shule ikiwamo madarasa matundu ya choo pamoja na madawati.

Katika mgawanyo wa fedha hizo, Wilaya ya Ikungi imepewa Sh. bilioni 1.47, Iramba Sh. bilioni 1.59, Itigi Sh.bilioni 1.39, Manyoni Sh.milioni 909, Mkalama Sh.milioni 925, Singida DC Sh. bilioni 1.351 na Manispaa ya Singida wamepata Sh. bilioni 1.371.

Serukamba, aliziagiza halmashauri zote mkoani hapa kuhakikisha zinaongeza umahiri katika usimamizi wa miradi mbalimbali ikiwemo wa mradi wa boost ili kuhakikisha inakamilika kwa wakati na kwa gharama zilizokusudiwa kabla ya mwisho wa mwaka wa fedha kumalizika.

Aliwaelekeza viongozi kusimamia na kutembelea miradi mara kwa mara ili kutatua changamoto ambazo zinaweza kuibuka wakati wa utekelezaji, huku akiwataka wakuu wa wilaya wote kukutana na wauza saruji ili kukubaliana gharama za ununuzi na ufikishwaji wa saruji katika maeneo ya kazi.

Hata hivyo, aliwataka wakurugenzi wa halmashauri kuwalipa kwa awamu mafundi watakaotekeleza ujenzi wa madarasa hayo huku akitoa tahadhari kwa mafundi ambao wamekuwa na tabia ya kutowalipa vibarua waliofanya nao kazi na kusababisha kazi kuchelewa.

# Wadaiwa kodi ya ardhi kuburuzwa mahakamani

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

WIZARA ya Ardhi Nyumba na Maendeleo ya Makazi imesema itawafikisha mahakamani watu wote wanaodaiwa malimbikizo ya kodi ya pango la ardhi pamoja na kukamata mali zao.

Pia imesema itabatilisha hati zao baada ya kuisha kwa kipindi cha msamaha wa Rais uliotolewa ifikapo Aprili 30 mwaka huu.

Mkuu wa Kitengo cha Kodi wa wizara hiyo, Denis Masami, alibainisha hayo juzi jijini hapa, alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari kuhusu ukusanyaji wa madeni ya pango la ardhi katika kipindi ambacho serikali ilitoa msamaha kwa wanaodaiwa kulipa bila riba.

"Rais Samia alitoa msamaha kwa waliolimbikiza malipo ya kodi ya pango la ardhi katika kpindi cha kuanzi Julai hadi Desemba mwaka jana ambapo watu 6,000 walijitokeza kutumia fursa hiyo na kulipa bila riba.

"Lakini watu wengi waliomba muda uongezwe na serikali kutoa msamaha kwa awamu ya pili ya kuanzia Machi hadi Aprili mwaka huu, ambapo hadi sasa watu 8,725 wamejitokeza kulipa bila riba,"alisema Masami.

Kadhalika alisema hadi sasa kiasi cha malimbikizo ya kodi ambacho kimeshalipwa ni Sh. bilioni 31.5 na kiasi cha riba ambacho kimesamehewa ni Sh. bilioni 21.3.

"Hivyo basi niwasihi wananchi kutumia fursa hii ya msamaha wa Rais Samia Suluhu Hassan, kulipa malimbizo ya madeni yao kodi ya pango la ardhi bila riba kwani muda ukifika wote watakaoshindwa kulipa tutawachukulia hatua ikiwamo kuwafikisha mahakamani na kushikilia mali zao na kubatilisha hati zao"alisema

Kamishna wa Ardhi Msaidizi Mkoa wa Dodoma, Jabir Singano, alisema katika kipindi cha msamaha wa Rais wananchi 1,200 wamejitokeza kulipa madeni yao.

"Katika mkoa wetu watu zaidi ya 1,200 wamejitokeza kulipa na kiasi cha Sh. bilioni 1.2 kimeshalipwa hadi sasa tunaendelea kuhimiza wote ambao bado wanadaiwa kulipa katika muda huu uliobaki ili kuepeka usumbufu utakaojitokeza," alisema Singano.

Aidha, alisema katika jitihada za kuongeza makusanyo Mkoa wa Dodoma umeendelea kutatua kero zilizokuwepo ikiwemo kukwama kwa malipo ya miamala ya maombi ya wateja.

Alisema: "Lakini pia kulikuwepo na shida ya upatikanaji wa namba za malipo hili pia tumelifanyia kazi ambapo tumetoa namba za malipo zaidi ya 4,050 kwa wateja kupitia timu yetu tuliyoiunda kulifanyia kazi suala hili lililokuwa kikwazo kwa wananchi wetu"



Mkuu wa Kitengo cha Biashara wa Benki ya Absa Tanzania, Bwana Melvin Saprapasen (kulia), akigawa chakula wakati wa futari, iliyoandaliwa na benki hiyo kwa wateja wake, jijini Dodoma juzi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Kampuni yabaini chanzo kipya cha mapato ya h'shauri

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

KAMPUNI ya Soza Limited, imebaini chanzo kipya cha mapato kinachoweza kuongeza mapato ya halmashauri nchini, ambacho hakileti migogoro wala maumivu kwa walipaji.

Akizungumza na waandishi wa habari pasipo kukitaja chanzo hicho, Mkurugenzi Mtendaji wa kampuni hiyo, Patrick Soza, alisema wamekuwa wakifanya utafiti wa vyanzo vipya vya mapato ili kuisaidia serikali kuongeza mapato yake.

"Tumepita takribani mikoa 24 na kufanya utafiti wetu na tumebaini kuwa serikali inapoteza mapato ya Sh.milini 20 kwa siku na Sh. milioni 600 kwa mwezi na Sh. bilioni 7.2 kwa mwaka.

"Baada ya kugundua chanzo hicho kipya cha ukusanyaji wa mapato hapa nchini tunaomba ushirikiano wa Wizara ya TAMISEMI, ili tupate kibari cha kukutana na halmashauri na manispaa hapa nchini ili kuweka makubaliano ya asilimia ambayo kampuni yetu itakuwa ikipata baada ya ukusanyaji wa mapato hayo"alisema

Alisema chanzo hicho ni kizuri, hakileti migogoro wala maumivu kwa walipaji nchini na wako tayari kukaa na wizara kutoa mchanganuo wao na utafiti waliofanya endapo watapatiwa kibari cha ukusanyaji wa mapato ya chanzo hicho.

"Kwa mantiki hiyo sisi kama Soza Company Limited, tumefanya utafiti na kuonyesha upotevu wa mapato ya serikali katika vyanzo mbalimbali na hiki ni kimojawapo tu katika vyanzo vilivyofanyiwa utafaiti"alisema

Kutokana na hali hiyo alisema wanaomba nafasi ya kuonana na Katibu Mkuu TAMISEMI, ili waweze kuongea naye juu ya jambo hilo kwani katika halmashauri na manispaa ushirikiano wanaopewa ni wa kutaka kuchukua mawazo yao na kuyafanyia kazi bila kuwashirikisha.

Alisema pamoja na jitihada ambazo wamezifanya bado wameshindwa kukutana na viongozi wakuu wa serikali hasa wa Ofisi ya Rais TAMISEMI ambayo ndiyo wenye mamlaka na serikali za mitaa.

Vile vile alisema kampuni hiyo imefanya utafiti wa mapato yanayopotea bila kukatwa kodi, kwamba wamebaini Sh. bilioni 2.3 zinapotea bila kukatwa kodi katika Halmashauri ya Manispaa ya Kigoma Ujiji.

Alisema: "Kwa siku Sh.miloni 6.5, kwa mwezi Sh. milioni 195 na kwa mwaka Sh. bilioni 2.3, hivyo tunaomba kuwasilisha taarifa yetu na kuonyesha chanzo hicho cha mapato ili tuweze kushirikiana kukusanya kodi ya serikali inayopotea kupitia chanzo hicho".





## TRA yatakiwa kuwafuatilia wadaiwa sugu ulipaji kodi

**Na Mwandishi Wetu**

WATENDAJI wa Mamlaka ya Mapato nchini (TRA), wametakiwa kufuatilia kwa karibu wadaiwa sugu katika masuala ya kodi, kupambana na wafanyabiashara wanaokwepa, kulipa kodi na kufanya udanganyifu katika shughuli zao.

Hayo yalisemwa na Mwenyekiti wa Kamati ya Baraza la Wawakilishi ya Uchumi, Sabiha Filfil Thani alipofanya mazungumzo na watendaji wa TRA.

Alisema, TRA inayo wajibu mkubwa katika utekelezaji wa majukumu yake kwani ni taasisi yenye kazi ya kukusanya kodi katika maeneo ya bandari na uwanja wa ndege kwa bidhaa zinazoingia nchini.

Hivyo, aliwataka watendaji wa taasisi hiyo kuhakikisha wanatekeleza majukumu yao vizuri na kupambana na wafanyabiashara wajanja ambao huikosesha nchi mapato.

"TRA ndiyo moyo wa nchi katika ukusanyaji wa mapato ya nchi ambapo tunawaomba kwa kutumia uwezo na uzoefu wenu kuhakikisha mnakusanya kodi zote na kuwadhibiti wafanyabiashara wajanja wanaokosesha mapato nchi"alisema.

Naibu Kamishna wa TRA, Juma Bakar alisema kupata mafanikio makubwa katika masuala ya ukusanyaji wa kodi, huku wakihamasisha wafanyabiashara kulipa kodi kwa hiari.

Aidha alisema wanashirikiana vizuri na wenzao TRA Zanzibar katika utekelezaji wa majukumu yao ambao wote kazi yao kukusanya mapato kwa maendeleo ya taifa.

"TRA kazi yetu kubwa sasa ni kutoa elimu kwa wafanyabiashara kuhusu suala zima la kulipa kodi kwa hiari ambayo matumizi yake ni kwa ajili ya kuleta maendeleo ya Watanzania"alisema.

Akizungumza katika mkutano huo Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango, Ali Suleiman Ameir alisema marekebisho makubwa ya sheria mpya ya TRA Zanzibar kwa kiasi kikubwa yataleta mageuzi makubwa ya ukusanyaji wa kodi na kufanya kazi hizo kwa ushirikiano na TRA.

Alisema: "Tumefanya marekebisho makubwa ya sheria na kuunda Mamlaka ya Mapato Zanzibar ambapo matarajio yetu tutafanya kazi pamoja na Mamlaka ya Mapato nchini TRA katika kazi za usimamizi wa kodi na ukusanyaji wa ma-

# WFP kuisapoti serikali uwezeshaji Wananchi kupata chakula lishe

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

SHIRIKA la Umoja wa Mataifa la Chakula Duniani (WFP) limeahidi kuunga mkono juhudi za Serikali ya Zanzibar katika kuwawezesha wananchi kupata chakula ambacho kitaimarisha lishe ya watoto na ukuaji wake.

Hayo yalisemwa jana na mwakilishi wa WFP Tanzania, Sara Gordon alipofanya mazungumzo na viongozi na watendaji wa Serikali ya Zanzibar katika Wizara ya Kilimo na Umwagiliaji Maji.

Alisema mahitaji ya chakula ni muhimu kwa jamii katika ukuaji na kulinda afya zao ambapo shirika hilo linashirikiana na serikali katika kuona mahitaji ya chakula yanapatikana.

Gordon alisema WFP imechukua juhudi za makusudi kufungua ofisi zake Zanzibar ili kufanya kazi kwa karibu na Serikali ya Zanzibar kuyafikia malengo endelevu ya dunia pamoja na Dira ya Maendeleo ya mwaka 2050.

Aidha, alifurahishwa na juhudi zinazochukuliwa na serikali ikiwemo Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali katika kuwapatia lishe wanafunzi waliopo shule za msingi hatua ambayo itasaidia na kujenga uwezo wa ufahamu.

"WFP linaunga mkono juhudi zinazochukuliwa na Serikali ya Zanzibar katika kuimarisha upatikanaji wa chakula pamoja na lishe kwa wanafunzi wa shule za msingi ikiwemo za vijijini hatua ambayo imesaidia kwa kiasi kikubwa kujenga uwezo wa wanafunzi hao"alisema.

Waziri wa Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo, Shamata Shaame Khamis, alisema serikali imeweka mikakati katika kujitosheleza kwa chakula kwa wananchi wake huku ikitekeleza miradi ya kilimo cha umwagiliaji maji shambani.

Alisema tayari yapo mashamba ya umwagiliaji maji ambayo yamekamilika kutengenezwa miundombinu ya umwagiliaji maji pamoja na kusambaza nishati ya umeme, hatua ambayo itasaidia upatikanaji wa maji ya kumwagilia mashambani.

Aidha, alipongeza shirika hilo kwa kuamua kufungua ofisi zake Zanzibar akisema hatua hiyo itasaidia kufuatilia shughuli zake ikiwemo za upatikanaji wa chakula na miradi yake kwa wananchi.

Alisema: "Nachukua nafasi hii kulipongeza WFP kwa kusaidia juhudi za miradi ya chakula kwa upande wa Zanzibar ambapo kitendo cha kufungua ofisi zake Zanzibar kitasaidia na kusukuma miradi yake kwa wananchi"



Wateja wa Benki ya KCB Tanzania, wakishiriki katika futari waliyoandaliwa na benki hiyo, Jijini Zanzibar juzi kwa lengo la kuboresha mahusiano na kuongeza ukaribu kwa ustawi wa biashara. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Walimu watakiwa kutumia mbinu za kisasa ufundishaji

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

WALIMU wa shule za maandalizi na msingi Zanzibar wametakiwa kutumia mbinu za kisasa katika ufundishaji ikiwamo wa vitabu ili kwenda sambamba na mabadiliko ya mitaala ya elimu ambayo imeanza kutumika.

Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali, Dk. Mwanakhamis Adam Ameir aliyasema hayo jana wakati akizungumza na walimu wa shule za msingi baada ya kuzindua vitabu vitakavyotumiwa na wanafunzi wa elimu ya maandalizi na msingi vinavyokwenda sambamba na mitaala mipya.

Alisema, Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali imeanzisha mitaala mipya ya elimu ya msingi na maandalizi kwa lengo la kuongeza kiwango cha ufaulu kwa wanafunzi kuelekea sekondari. Alifahamisha hayo ndiyo maboresho makubwa yanayofanywa na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali kwa ajili ya kuleta mageuzi makubwa katika sekta ya elimu na kuwawezesha wanafunzi kufaulu kwa kiwango cha juu. Alisema mageuzi hayo yanakwenda sambamba na ujenzi wa shule za ghorofa ambazo zitapunguza msongamano wa wanafunzi pamoja na kuweza kusoma katika mkondo mmoja tu wa asubuhi.

"Hiyo ndiyo mikakati yetu inayokwenda sambamba na maboresho ya sekta ya elimu Zanzibar na kuwawezesha wanafunzi kupata ufaulu mkubwa kuelekea sekondari"alisema.

Mkurugenzi wa Elimu ya Msingi na Maandalizi, Fatma Mode Ramadhan alisema katika kuelekea mitaala ya elimu ya msingi wizara imetayarisha vitabu ambavyo vitatumiwa kwa wanafunzi hao ili kuwawezesha kujua mbinu za matumizi ya vitabu.

Hivyo, aliwataka walimu waliopewa mafunzo juu ya mitaala mipya kusomesha kwa kuzingatia muongozo huo ili kuona wanafunzi wanapata ufaulu bora kuelekea elimu ya sekondari.

Alisema: "Hayo ndiyo matarajio yetu mapya kuona kwamba walimu wanatumia vitabu kwa ajili ya kufundisha wanafunzi mbinu za uchambuzi hatua ambayo itawawezesha kupata ufaulu mzuri"



TESSY
UKURASA 12



# HUYU HAPA

MWANAMITINDO na muigizaji wa Bongo Muvi, Hamissa Mobetto, amemtambulisha rasmi mwanamume ambaye kwa sasa wanakula maisha katika ulimwengu wa kimapenzi.

Hamissa ambaye ni mama wa watoto wawili, amesema baada ya kuishi singo kwa muda mrefu, ameamua kuingia katika maisha ya mapenzi na mwanaume ambaye hakutaka kutaja jina lake.

Amesema mchakato wa uhusiano huo unakwenda vizurui na pengine wanaweza kufunga ndoa baadaye.

Hata hivyo, mwanamume huyo amemweka mbali na watoto wake kutokana na wawili hao kutofikia hatua fulani ambayo itaweka uhalali wa kuwa karibu nao.

"Watoto wangu hawajawahi kuniona na mwanaume wangu, wakati mwingine wananiuliza lakini sitaki kuwapa mawazo kwa sababu unaweza kuwa na mtu ambaye sina uhakika naye na kuwapa matatizo watoto," amesema.

Amesema mpenzi wake huyo hana kawaida ya kumsumbua kwa kumpigia simu kila wakati kutokana na muda mwingi kuwa na kazi nyingi.

"Mpenzi wangu hana kawaida ya kunipigia simu mara kwa mara kwa sababu ana kazi nyingi, lakini ana upendo mwingi kwangu na watoto wangu licha hajawahi kuwaona," ameongeza kusema.

Hata hivyo, amesema ikifikia hatua ya kufunga ndoa haitakuwa na pingamizi kwake kwa sababu anampenda kwa dhati.



BASI SAWA

## Coy Mzungu bado hajaeleweka



MCHEKESHAJI maarufu nchini, Coy Mzungu, amekiri kwamba wako kwenye mgogoro na Diamond Platumz kiasi ambacho ameamua kukaa pembeni.

Coy Mzungu hakueleza sababu zinazomfanya yeye na Diamond kutoelewana, lakini inaelezwa kuwa wawili hao hawafanyi kazi pamoja katika kundi la Cheka Tu.

Hata hivyo, mpaka sasa kwenye akaunti ya Instagram ya Diamond anamtambulisha kama MD wa Cheka Tu, licha ya kuwa na mvutano na msanii huyo.

## Blackxtz asikitikia tuzo TMA

MWONGOZAJI wa video za muziki kutoka Tanzania Blackxtz amesema amehuzunishwa kuona wakongwe wameachwa



katika tuzo za TMA, badala yake wameshindanishwa wachanga pekee.

Amesema kuna changamoto katika kamati ya uteuzi ya wasanii wanaogombea tuzo hizo, na badala yake inaleta maswali mengi yasiyo na majibu katika mchakato huo.

"Kamati ya tuzo za TMA haina weledi katika kuthaminisha kwa sababu inafanya kazi bila malengo wala kujua nini wanachokifanya. Natamani kuwa katika tuzo lakini kutokana na changamoto zinazoonekana zinaweza kukuangusha," amesema Blackxtz



## SHILOLE AMEWAKOMESHA

MWANAMUZIKI wa Bongo Fleva, Shilole, amewajia juu wasanii wa kiume wanaolalamika kutokuwemo katika tuzo za TMA, kuacha kupiga kelele kwani kinachofanyika kiko wazi.

Amesema wengi wanaolalamikia tuzo hizo ni wasanii wa kiume ambao wamezoea kubebwa, hivyo amewataka kufanya kazi kwa bidii wataonekana.

"Watoto wa kiume fanyeni kazi, udananda utawaponza, ndio mimi Shishi Master kabisa napiga miguu yote," amesema Shilole.



## Nusura Tessy yampate mabaya

MPAMBAJI wa video za muziki, Tessy, amesimulia jinsi alivyompata mgeni nyumbani kwake na kumpa balaa lilohatarisha maisha yake.

Tessy ambaye ni mama mtoto wa mwanamuziki wa Bongo Fleva, Aslay, amesema mdogo wake alikwenda kumtembelea nyumbani kwake akiwa na simu ambayo ililipuka wakati ikichajiwa.

"Simu ilikuwa kwenye chaji ililipuka ghafla na kuunguza sofa, nawaombeni tusilale na simu kwenye chaji ni hatari. Kama ingekuwa usiku tungekufa kwani tusingejua kinachoendelea," amesema Tessy.

## HUSSEIN JUMBE KAACHA HIZI..

**Na Adam Fungamwango**

JUMATATU iliyopita, tasnia ya muziki wa dansi nchini ilipata pigo baada ya kuondokewa na mmoja wa wanamuziki wake mahiri waliobaki, Hussein Jumbe.

Mwanamuziki huyo alifariki dunia kwenye Hospitali ya Amana Ilala jijini Dar es Salaam alipokuwa amelazwa kwa ugonjwa wa kifua.

Alizikwa Jumanne kwenye makaburi ya Kisutu jijini Dar es Salaam na kuacha simanzi kubwa kwa wadau na mashabiki wake na muziki wa dansi pia.

Anakumbukwa zaidi kwa kupigia bendi kubwa za Msondo Ngoma Music, DDC Mlimani Park Orchestra, pamoja na Tanzania One Theatre maarufu kama TOT Plus Band.

Historia ya mwanamuziki huyo inaonyesha kuwa ameshawahi kupigia pia bendi za Asilia Jazz, Tabora Jazz na Mikumi Sound.

Kote alikopitia alitunga na kuimba nyimbo nyingi, zingine zikitungwa na wenzake.

Hizi ni baadhi ya nyimbo tano ambazo kwa kiasi kikubwa zilimfanya awe mwanamuziki maarufu, akijizolea mashabiki kila kona ya nchi.

**Nachechemea-DDC Mlimani Park**

Ilikuwa ni katikati ya miaka ya 1990 alipoibuka na kibao kiitwacho 'Nachechemea' ambacho ndiyo naweza kusema kilimtoa mwanamuziki huyo kutoka mwanamuziki wa kawaida na kuwa staa.

Ni wimbo uliopendwa na kila aliyekuwa anausikiliza, si mtoto, mkubwa, mwanaume, mwanamke, kijana na mzee. Kila mara wakati wa uhai wake alisisitiza kuwa kilikuwa ni kisa cha kweli. Wakati akiumwa kuna watu walivumisha kuwa amefariki dunia, na watu wakamiminika nyumbani kwake kwenye msiba wakati yeye akiwa mgonjwa kitandani. Ndiyo maana alipopona alitunga wimbo huo ambao baadhi ya maneno ni haya.

"Na wengine wakatangaza nimeaga dunia, na sanduku la gharama wakanichongea, kwa mapenzi yake jalali leo nachechemea."

**Mrithi wangu Isaya-DDC Mlimani Park**


Ilikuwa ni mwanzoni mwa miaka ya 2000, alipotoka na kibao chake kiitwacho 'Mrithi Wangu Isaya.'

Wimbo huu uliendelea pale alipoishia kwenye wimbo wa 'Nachechemea.' Nao ulitokea kuwa maarufu sana.

"Isabella kanikimbia nyumbani, katoroka na mtoto wangu wa pekee, mrithi wangu wa baadaye. Mtoto wangu wa kiume, Isaya." Ni baadhi ya maneno yaliyomo kwenye wimbo huo.

**Nani Kaiona Kesho-TOT Plus**

Miaka hiyo hiyo ya 2000, Jumbe alilipa kisogo kundi la Sikinde na kwenda kujiunga na TOT Plus. Moja ya nyimbo zilizomfanya aendelee kuwa mmoja wa wanamuziki staa nchini ni 'Nani Kaiona Kesho.' Ni wimbo ambao hata alipoondoka Sikinde walikwenda kuurekodi kwa jina la "Nani Kauona Mwaka.' Maudhui ni mamoja. Watu wanapambana sana kujionyesha na kuchanga pesa kufanya mazishi ya gharama, wakati mgonjwa alikuwa anahitaji 'dripu' tu, lakini alikosa pesa.



**Sarafina-TOT Plus**

Sitaki kuusimulia sana wimbo huu wa 'Sarafina', lakini hebu utafute na usikilize sauti safi ya Jumbe kwenye wimbo huu aliouimba akiwa TOT, hasa pale anapouanzisha "Umempata huyooo."

**Mapenzi ya Siri-Talent Band**

Huu pia ni wimbo maarufu, na uzuri zaidi hata vijana wa kizazi cha sasa wanaujua. 'Mapenzi ya Siri', alirekodi akiwa na bendi yake binfsi aliyoita Talent Band.

Katika wimbo huo anampasha mpenzi wake ambaye hataki mapenzi yao yawe hadharani kila mtu afahamu, anataka iwe siri kitu ambacho yeye mwenyewe hakitaki.

FILAMU

## Sophia Madeni: Ushetani mikopo kaushadamu

**Na Adam Fungamwango**

KUNA tabia fulani kwa sasa imezuka kwa baadhi ya kinamama kukopa pesa kwenye taasisi za ukopeshaji, vikoba, au watu binafsi wanaofanya shughuli hizo na kuzitumia kwa mambo ya starehe kama vile sherehe za kutunzana, rusha roho na mengine yaliyofanana na hayo.

Baadhi ya kinamama huona fahari sana kusifiwa kuwa sherehe yake imefanya, au ametunza vitu vya gharama kuliko wenzake, badala ya kufanya vitu vya maendeleo.

Hii imewarudisha nyuma sana baadhi ya kinamama, kiasi cha hata ile maana ya taasisi hizo hukopesha inakuwa haipo tena.

Kuna funzo linapatikana kwenye filamu hii tunayoitazama leo, inaitwa 'Sophia Madeni.'

Imechezwa na kina Dora Martin, Rayuu Chande, Nassor Chilumba, Verena Mathayo na wengineo.

Sophia ni msichana anayekopesha pesa mtaani kwa akinamama wanaotaka kujiendeleza. Mwenyewe anakopesha akinamama wenye biashara zao ili wazidi kupanua mitaji yao, lakini pia wale wanaotaka kuanza.

Siwajibu ni mmoja kati ya wanufaika. Ana shoga yake aitwaye Verena, Na yeye anataka pesa. Anadai anataka kwa ajili ya kufanyia biashara. Ukweli sivyo hivyo. Jirani yake ana sherehe, hivyo anahitaji pesa kwa ajili ya kununua zawadi za kwenda kumtunza.

Anamfuata Siwajibu ampeleke kwa Sophia. Wanapofika, mkopeshaji anamuuliza kama ana biashara na kumsihi pesa anazomkopesha zikafanyie biashara na si vinginevyo.

Verena alihitaji shilingi laki tatu. Akapewa. Muda wa kulipa ukafika, lakini hakuwa na pesa yoyote ya kulipa. Alikwenda kukopa huku mumewe akiwa amekataa kwa sababu alijua hana biashara yoyote ambayo ingemuwezesha kulipa.

Verana alimpa mumewe pesa akaenda kununua zawadi kwa ajili ya kumtunza jirani yake kwenye sherehe za kutunzana.

Sophia sasa amecharuka, anataka pesa zake kwa sababu kila akimsaka Verena amekuwa ni mtu na kumkimbia, kubadilisha njia, kufunga milango, na kila aina ya hila.

Mume akasema hawezi kulipa kwa sababu alishamkanya tangu mapema na alijua mkewe alikuwa anazitaka pesa hizo kwa ajili ya nini.

Hali ikazidi kuwa mbaya kiasi cha Sophia sasa kwenda kwa mjumbe na Mwenyekiti wa Serikali za Mitaa. Ikawa imebaki polisi tu. Mume naye kachachamaa anataka kutoa talaka. Verena alilia na kuomba msamaha kuwa hatorudia tena. Mume akaamua alipe na kumuonya asifanye hivyo tena. Sophia akamkumbusha Verena kuwa pesa za mkopo hazichezewi ngoma na vijora pambe, bali ni za kufanyia biashara.





# Mercy kumbe mama kijacho?

MSANII maarufu wa Injili kutoka Nigeria, Mercy Chinwo, ameibua minong'ono kuwa ni mjamzito baada ya kuonekana kwenye video ya wimbo wake mpya unaoitwa 'Wonder'.

Katika video hiyo ameonekana akiwa amevalia nguo ya kijani inayotiririka inayoonekana kuficha tumbo lake.

Mashabiki waligundua haraka uwezekano wa msanii huyo kuwa na ujauzito, na wengi waliingia kwenye mitandao ya kijamii kuelezea furaha na pongezi zao.



## Canon atamani mtoto na Taylor

MWANAMUZIKI na mwendeshaji wa kipindi cha TV, Nick Cannon, ameelezea ndoto yake ya kupata mtoto na mwimbaji Taylor Swift.

Cannon alitangaza hamu yake hiyo kwenye  kipindi cha 'The Howard Stern Show', akikiri kwamba hana mipango ya haraka ya kuongeza watoto wake wakubwa, lakini angebadili mawazo yake ikiwa Swift angetaka kuanzisha familia naye.

"Kwanza kabisa, yeye ni mtunzi wa ajabu wa nyimbo. Ninachopenda kuhusu Taylor Swift ni kwamba amekuwa katika mazingira magumu sana na wazi kwa muziki wake wote ni mzuri na ningependa kuwa na mtoto naye."

## Lojay umeambiwa mapenzi yanaua

MWIMBAJI na mtunzi wa nyimbo wa Nigeria, Lekan Osifeso Jnr. maarufu kama Lojay, amefichua kuwa wanawake wamemvunja moyo mara nyingi.

Akishiriki kwenye kipindi cha podikasti ya 'Moni Talks', iliyoandaliwa na Moni Osibodu. Mwimbaji huyo alikiri kuwa mapenzi yalimuumiza mara nyingi.

"Mimi ni mwanamume, siku zote nimekuwa mvulana wa kimapenzi. Sidhani kwamba hilo litabadilika. Lakini wakati huo huo anaumizwa na wanawake mara nyingi," amesema.





## Yul kafuta zote Instagram

MWIGIZAJI maarufu wa Nollywood, Yul Edochie amefuta machapisho yake yote kwenye ukurasa wake wa Instagram.

Hatua hiyo ameichukua kutokana na kifo cha mwanawe wa kwanza wa kiume na mkewe wa kwanza May, Kambilichukwu, aliyeaga dunia Machi 30, mwaka huu.

Mwigizaji huyo mtata ambaye amekaa kimya kuhusiana na suala hilo kwenye mitandao ya kijamii, inasemekana aliwataka polisi kuangalia tukio hilo la kusikitisha.

## Victony muombe Mungu

MWIMBAJI wa Nigeria, Anthony Victor, maarufu kama Victony, amefichua siri yake kuwa alikuwa katika hali ya mahututi kwa siku nne baada ya kupata ajali mwaka 2021.

Msanii huyo aliponea chupuchupu na kuwa katika hali mbaya kufuatia gari alilokuwa akisafiria kuacha njia na kupata ajali.

"Nilipotoka tu kwenye klabu, tulipokuwa tunarudi, nililala. Nilikuwa nimechoka. Nilipoamka, nilikuwa hospitalini, niliuliza nini kilitokea? Amesema.










Mwezeshaji kutoka Mradi wa Ujana Salama wa Shirika la Femina Hip, Stellah Mbuya (kushoto), akiwatambulisha kwa wananchi baadhi ya vijana 180 kutoka kata sita za Wilaya ya Muheza, mkoani Tanga, waliopatiwa mafunzo ya kupambana na ukatili wa kijinsia katika eneo la Majengo Shimoni juzi. **PICHA: STEVEN WILLIAM**

# Mstahiki Meya akerwa tabia kutelekeza watoto

**Na Cynthia Mwilolezi,** ARUSHA

MSTAHIKI Meya wa Halmashauri ya Jiji la Arusha, Maxmilian Iranqhe, amekemea tabia ya kuwatelekeza watoto, kukwepa majukumu ya kulea akisema wanasababisha ongezeko la watoto wa mitaani.

Alitoa onyo hilo jana wakati akizungumza katika Siku ya Kimataifa ya Mtoto wa Mtaani iliyoandaliwa na kituo cha kulea watoto wa mtaani cha Amani kilichopo Kaloleni jijini Arusha

Alisema: "Watoto hawa hawakuchagua kuwa mitaani wala kufanya kazi ngumu nje ya uwezo wao, bali ni wazazi pande mbili walikubaliana kwa mapenzi yao kuwaleta watoto hawa kwa kuwa malezi ni jukumu la kila mzazi, hivyo naonya wale wote wanaokwepa majukumu yao waache tabia hii haileti afya kwa jamii".

Mratibu wa Kituo cha Amani jijini Arusha, Naomi Kimaro, alisema kituo hicho kimekuwa kikihudumia watoto katika nyanja mbili ambazo ni watoto wa mtaani na watoto wa makazi salama kwa kushirikiana na wadau wengine.

Alisema kwa upande wa makazi salama wamekuwa wakiokoa watoto ambao wanapelekwa kwenye madawati ya polisi jamii, ustawi wa jamii pamoja na wasamaria wema, kwamba huwahudumia na kukaa nao kwa miezi sita wakipatiwa huduma na kurudishwa katika familia zao.

"Hapa kituoni tuna uwezo wa kuhifadhi watoto 22, tunakaa nao wakati tukiendelea kufuatilia familia zao, huku wakiendelea kupatiwa huduma mbalimbali hata wakiondoka hapa, tunaendelea kuwafuatilia ili kuhakikisha wanapata huduma zote wanazostahili wakiwa kwenye familia zao,"alisema .

Aidha, alisema kwa kipindi cha mwaka jana walifanikiwa kuokoa watoto wa mtaani 126 na kuwapatia huduma ya elimu na kurudishwa katika familia, huku watoto 96 wa makazi salama wakifanikiwakuokolewana kurudishwa katika familia zao.

Vilevile waliiomba serikali kutenga bajeti kwa watoto wanaoishi na kufanya kazi mtaani, ili wapate mahitaji muhimu bure kwa kuwawajibisha wazazi wanaokwepa majukumu ya kulea watoto na kuchangia kuwapo kwa ongezeko kubwa la watoto wa mitaani.

Akisoma risala ya maadhimisho hayo, Joshua Dunkan, mmoja wa watoto wanaoishi mtaani alisema mtaani siyo sehemu salama pa kuishi japo zipo sababu mbalimbali za kifamilia zimesababisha wao kujikuta katika mazingira magumu.

# Maofisa TEHAMA, waraibu dawa kulevya wapewa mafunzo

**Na Oscar Assenga,** TANGA

MAOFISA wa Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA), watoa huduma wa kitengo kinachoshughulika na waraibu wa dawa ya kulevya kutoka Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Tanga ya Bombo, wamepatiwa mafunzo ya uboreshaji wa mazingira ya mtoa huduma. Mafunzo hayo yalitolewa na Mkuu wa Idara ya Udhibiti Ubora wa Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Tanga ya Bombo, Joseph Nzige ambaye alisema yanafaida ikiwamo kuongeza ufanisi wa utaoji wa huduma kwa mazingira bora yaliyopangiliwa.

Akizungumza jana wakati wa mafunzo hayo, Nzige alisema pia yatasaidia kuongeza usalama wa afya ya mtoa huduma (mteja) mgonjwa ikiwamo kupunguza ucheleweshaji wa utoaji wa huduma unaosababishwa na mazingira hafifu Aidha aliwataka watumishi wa vitengo hivyo kuhakikisha wanatumia mafunzo ili yaweze kuwa na tija katika kuboresha utendaji na ufanisi wa kazi zao kila siku.

Hata hivyo alisema mafunzo yatakuwa yakitolewa mara kwa mara kwenye hospitali hiyo ili yaweze kuongeza ujuzi na ufanisi kwa ajili ya uboreshaji wa mazingira ya mtoa huduma.

Naye Mkuu wa Kitengo cha TEHAMA katika hospitali hiyo, William Masika, ambaye ni miongoni mwa washiriki wa mafunzo alisema mafunzo hayo ni muhimu kwa ajili ya kuongeza ufanisi wa utendaji katika shughuli zao za kila siku.

# Serikali kutaifisha mifugo itakayoingia Uwanja wa KIA

**Na Mary Mosha ,** HAI

SERIKALI imesema itachukua hatua ya kutaifisha mifugo inayoingizwa kiholela katika eneo la hifadhi ya mazingira kwenye Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Kilimanjaro (KIA).

Hayo yalisemwa na Mkuu wa Mkoa wa Kilimanjaro, Nurdin Babu, wakati akizindua kampeni ya upandaji wa miti 10,000 katika eneo la kuzunguka eneo la KIA inayoendeshwa na Kampuni ya Uendelezaji na Uendeshaji wa Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Kilimanjaro (KADCO).

Hata hivyo aliwataka wakuu wa wilaya na wakurugenzi wa halmashauri za wilaya zote sita za mkoa huo kutekeleza kwa vitendo agizo la kupanda miti milioni 1.5 kila mwaka.

"Tangu serikali itangaze kampeni ya kupanda miti milioni 1.5 ungekuta hakuna hata sehemu ya kupita, nitakuja huko wilayani kwenu mnionyeshe miti mliyopanda, jambo hili sitalifumbia macho kwa kuwa miti itasaidia kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi,"alisema.

Aidha, alipongeza KADCO kwa kubuni mradi ya kutunza mazingira ya uwanja huo kwa kuwa itasaidia kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi sambamba na kuwa kivutio kwa wageni kutoka ndani na nje ya mkoa.

Kadhalika alisema uwanja huo ni mali ya serikali na kwamba mifugo itakayokuwa inaingizwa kwenye eneo ni ukiukwaji wa sheria za nchi.

Alisema katika kulinda mazingira ya eneo la uwanja huo serikali imetoa fidia ya zaidi ya Sh.bilioni 11 ikiwa ni sehemu ya kumaliza mgogoro kati ya wananchi wanaozunguka uwanja huo kwa zaidi ya miaka 21 sasa.

Vilevile aliwataka wakurugenzi wa halmashauri za wilaya kuweka utaratibu maalumu Kwa kila mwananchi anayejenga makazi kuonyesha miti mitatu katika eneo lake.

Mkurugenzi wa KADCO, Christen Mwakatobe, alisema hali ya mazingira katika uwanja huo siyo nzuri kwa kuwa mwanzoni mwa mwaka 1980 serikali kwa kushirikiana na wadau wa maendeleo duniani ambao ni FAI na JICA walianzisha mradi wa kupanda miti KIA.

Alisema kupitia kampeni hiyo, KADCO imeandaa mpango endelevu wenye kauli mbiu isemayo 'Ifanye KIA kuwa ya kijani'.

## TULIKOTOKA, TULIPO & TUNAKOKWENDA...

# Miaka 39 ya Sokoine mwasisi wa daladala

## -Akaamuru mabasi ya makampuni kubeba abiria
## -Akavunja urasimu wa Shirika la Ugawaji

**Na Adam Fungamwango**

KWA vijana wa kizazi cha sasa, inawezekana kabisa baadhi yao wanapanda daladala, lakini hawajui zilianza vipi. Hizi daladala ambazo zinaonekana leo kutoka na kwenda sehemu mbalimbali kwenye jijini la Dar es Salaam, mwasisi wake ni Edward Moringe Sokoine.

Vijana wa sasa wanaweza kushangaa kwani wanachofahamu ni kwamba Sokoine alikuwa mwanasiasa na Waziri Mkuu mara mbili, tangu tarehe 13 Februari 1977 hadi 7 Novemba 1980, tena tangu tarehe 24 Februari 1983 hadi kifo chake mwaka 1984, inakuwaje tena yeye ndiye mwanzilishi wa usafiri huu wa daladala tunazoziona leo?

Ni kweli, mbali na mambo mengi sana mazuri ambayo Sokoine ameyafanya kwenye nchi hii ambayo vijana wengi wanayasoma sana kwenye siasa, lakini moja ambalo halitosahaulika ni hili.

Jumatano iliyopita, Tanzania iliadhimisha miaka 39 ya kifo cha shujaa huyo, ambaye alifariki kwa ajali ya gari Aprili 12, 1984.

Wakati akitoka bungeni, gari lake lilipata ajali maeneo ya Dumila, Dakawa Morogoro akitoka Dodoma bungeni, gari lake aina ya Benz liligongwa na Toyota Land Cruiser lililokuwa likiendeshwa na Dumisan Dube, raia wa Afrika Kusini, aliyekuwa akiishi kwenye kambi ya Mazimbu Morogoro. Sokione akafariki papo hapo.

Februari 23, 1983, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania wakati huo Mwalimu Julius Kambarage Nyerere, alimteua tena kuwa waziri mkuu, baada ya afya yake kuimarika. Aliporudi tena ofisini, akakuta hali ya usafiri Dar es Salaam ni mbaya sana.




Shirika la Usafiri Dar es Salaam (UDA), lilikuwa limeelewa na abiria, likiwa na mabasi machache kiasi kwamba halikuweza tena kumudu biashara hiyo, lakini sheria ya nchi wakati huo haikuruhusu watu binafsi kumiliki mabasi, ndipo yeye kama Waziri Mkuu, akawaita wafanya biashara wenye kuweza kununua mabasi ili watoe huduma ya usafiri, akipendekeza pia sheria hiyo ibadilishwe.

Ndipo wakajitokeza wafanyabiashara wengi wananunua mabasi ya usafiri na kuanza kutoa huduma hadi leo hii.

Wakati mabasi ya UDA yalikuwa yakitoza nauli shilingi tatu, mabasi ya watu binafsi yalipoanza wao walianza na nauli ya shilingi tano. Wakati huo shilingi tano ya Tanzania ilikuwa sawa na dola moja ya Kimarekani, na mtaani vijana wa mjini ile safaru moja ya shilingi tano walikuwa wanaiita dala, wakiwa na maana ile safaru thamani yake ni sawa na dola moja.

Makonda na utingo walianza kuitia abiria walisema, “Kariakoo nauli dala”, wakiwa na maana ya shilingi tano, hapo ndipo lilipozaliwa jina la daladala.

Mtu akitaka kwenda kupanda usafiri wa mabasi binafasi basi atamwambia mwenzake kuwa anakwenda kupanda daladala, ndiyo likawa jina la mabasi hayo ukitaka kuyatofautisha na mabasi ya UDA, yaliyokuwa yakimilikiwa na Shirika la Usafiri Dar es Salaam chini ya usimamizi wa serikali.

Sokoine pia aliamuru mabasi ya wafanyakazi wa makampuni na mashirika yaliyokuwa mengi mno wakati huo kuchukua pia kuchukua abiria.

Kilichofanyika ni kwamba baada ya kupeleka wafanyakazi maofisini, mabasi hayo hayakutakiwa kukaa yadi na kusubiri kuwarudisha majumbani jioni, bali yalitakiwa kupita vituoni kupakia abiria na kuwasafirisha, huku wakiwatoza kiasi kile kile cha pesa cha shilingi tano.

Na hata jioni waliporejesha wafanyakazi majumbani, kazi yao iliyobakia ilikuwa hiyo, hadi saa mbili usiku.

Kusema kweli ilisaidia kuondoa kero na hali mbaya ya usafiri Dar es Salaam kiasi cha kumalizika kabisa mpaka sasa ikawa abiria wanachagua mabasi ya kupanda badala ya kusubiri kwa masaa mawili au matatu kama ilivyokuwa mwanzo.

Sokoine pia anakumbukwa kwa kuondoa urasimu wa Shirika la Ugawaji lililokuwa ndilo lenye dhamana ya kugawa bidhaa kama unga, ngano, mchele kwenye maduka jijini Dar es Salaam, lakini hali ya chakula ilipokuwa mbaya miaka hiyo ya katikati ya 1980, Sokoine aliamuru mahindi kutoka mikoani yaletwe Dar na watu binafasi na wauze madukani, wananchi wanunue wakasage wenyewe unga, badala ya kusubiri unga madukani ambao haupo, au unaletwa mara moja kwa wiki na kugaiwa kwa mgao.

Hali hii nayo ilianza taratibu kupunguza adha ya chakula na ndipo Dar kukawa na mashine nyingi za kukoboa na kusaga, njaa ikaanza kuisha.

Huyu ndiye sokoine, mwanasiasa anayekumbukwa mno na Watanzania wengi kutokana na uzalendo wake ambao si wa kuigiza, bali wa kutoka ndani ya moyo kwani hata yeye mwenyewe alikuwa anauishi, kwani hakuwa mtu wa kujilimbikizia mali, na hata alipofariki mali kubwa alizokuwa nazo ni ng’ombe za urithi.

Baada ya ajali, mwili wake uliletwa Dar Es Salaam kisha ukapelekwa uwanja wa ndege kwa ajili ya kusafirisha kwenda Monduli Arusha kwa mazishi.

Wamiliki wa daladala walitoa usafiri bure kwa watu waliotaka kwenda uwanja wa ndege kuusindikiza mwili wa Sokoine, mtu aliyewapa dili la biashara ya kusafirisha abiria.



Marehemu, Edward Moringe Sokoine.



# Waziri agoma kujiuzulu, kisa 'mbakaji facebook'

**CAPE TOWN,** AFRIKA KUSINI

WAZIRI wa Sheria wa Afrika Kusini, Ronald Lamola, amekataa kujiuzulu katika sakata la mtuhumiwa wa ubakaji aliyetoroka gerezani na kukamatwa nchini Tanzania.

Lamola, liwaambia wabunge kwamba hatajiuzulu kutokana na tukio hilo alilofanya mbakaji na muuaji, Thabo Bester, aliyetoroka kutoka katika gereza la kibinafsi.

Bester alisafirishwa hadi Afrika Kusini Alhamisi kwa ndege maalum ya kukodi, kufuatia kukamatwa kwake nchini Tanzania wiki iliyopita.

Mtu huyo anajulikana kama mbakaji wa Facebook kutokana na kutumia mtandao wa kijamii kuwarubuni wahasiriwa wake. Mpenzi wake, daktari maarufu Nandipha Magudumana, ambaye alikamatwa naye, pia alirejeshwa Afrika Kusini

Waziri aliomba radhi kwa udhaifu wa gereza na alisisitiza alichukua jukumu kamili.

"Sitajiuzulu kwa sababu nilifanya kile nilichopaswa kufanya," Ronald Lamola aliiambia kamati ya bunge.

Alisema idara ya magereza ina wajibu wa kuhakikisha wafungwa wanawekwa jela hadi mwisho wa vifungo vyao.

**BBC**

# Korea Kaskazini yarusha kombora lenye nguvu

**PYONGYUNG,** KOREA KASKAZINI

KOREA Kaskazini imesema ilifanyia majaribio kombora jipya la balestiki linalotumia mafuta na uwezo wa kufikia mabara mengine.

Shirika la Habari la serikali lilipongeza uzinduzi huo uliofanyika Alhamisi, lakini nchini Japan ilisababisha kuwepo kwa agizo fupi la kuhamishwa kwa watu.

Makombora ya aina hiyo yanayotumia mafuta yanaweza kurushwa kwa haraka zaidi kuliko ya kawaida, hivyo kuyafanya kuwa vigumu kuyagundua na kuyazuia.

Kiongozi wa chi hiyo, Kim Jong Una, alisema jaribio hilo litawafanya wapinzani wake kukabiliwa na woga na wasiwasi.

Korea Kusini, ilisema teknolojia iliyoonyeshwa sio mpya na Kaskazini itahitaji muda na juhudi zaidi ili kuunda ICBM ya mafuta yenye nguvu inayofanya kazi kikamilifu.

Ilielezwa Kim alisimamia jaribio hilo pamoja na mke wake, binti yake na dada yake.

Pia, alisema silaha ya majaribio, inayojulikana kama Hwasong-18, itasaidia mkakati wa kijeshi wa Korea Kaskazini.

Uzinduzi huo uliofanyika Alhamisi asubuhi ulilenga kuthibitisha utendaji kazi wa injini za msukumo wa juu, teknolojia ya kutenganisha jukwaa na kutegemewa kwa mifumo mbalimbali ya udhibiti wa utendaji.

Tukio hilo ni mara ya kwanza kwa Korea Kaskazini kufanya majaribio ya ICBM ya mafuta baada ya miaka mingi ya majaribio ya makombora ya masafa mafupi ya mafuta.

Imefanyia majaribio ICBM mbalimbali, lakini la sasa liliendeshwa na vichochezi vya kioevu ambavyo haviwezi kuwashwa kwa muda mrefu.

Wataalamu walisema ni mafanikio makubwa katika mpango wake wa silaha, kwani ICBM za mafuta ni imara zitaiwezesha Korea Kaskazini kuishambulia Marekani bila onyo lolote.

Uzinduzi huo ulizua sintofahamu kaskazini mwa Japani, ambapo agizo la kuwahamisha watu lilitolewa na kisha kubatilishwa ndani ya dakika 30.

Shule katika kisiwa cha Hokkaido nchini Japani zilichelewesha kuanza kufundisha na baadhi ya huduma za treni zilisitishwa.

**BBC**




Vikosi vya usalama na uokoaji wakikusanyika kando ya kiwanda cha nguo kilichoanguka katika eneo la viwanda huko Karachi, Pakistan, jana baada ya kuteketea kwa moto. **PICHA: AFP**

# Aliyevujisha nyaraka nyeti za Marekani akamatwa

**WASHINGTON,** MAREKANI

MAOFISA wa shirika la upelelezi wa ndani la Marekani (FBI) wamemkamata kijana wa miaka 21, anayeshukiwa kuhusika na uvujishaji wa nyaraka za siri.

Nyaraka zilizovujishwa ikiwamo vita vya Ukraine na Marekani kuwachunguza washirika wake.

Akizungumza na vyombo vya habari, Mwanasheria Mkuu wa Marekani Merrick Garland alimtaja mshukiwa huyo kuwa ni Jack Teixeira, ambaye ni mfanyakazi katika jeshi la anga la walinzi wa taifa na kiongozi wa kundi la mtandaoni ambako hati hizo zilivujishwa kwa mara ya kwanza.

Kukamatwa kwake kulitangazwa moja kwa moja na Televisheni, kunafuatia kukamilika kwa uchunguzi wa wiki nzima uliochochewa na ripoti za vyombo vya habari vya Marekani katika mojawapo ya uvujaji mbaya zaidi wa taarifa za siri tangu sakata la Edward Snowden, mwaka 2013.

Ofisi ya jeshi la anga la walinzi wa taifa la Marekani, lilisema kuwa Teixeira alijiunga mwaka 2019, na alikuwa ni mtaalamu wa Tehama ambaye alikuwa amefikia kiwango cha wafanyakazi wa daraja la kwanza.

Wizara ya ulinzi ya Marekani Pentagon ilisema kuvuja kwa taarifa hizo kunaweka hatari kubwa kwa usalama wa taifa hilo.

Kukamatwa kwa Teixeira, kulitokea siku moja baada ya gazeti la The Washington Post kuripoti kuwa mamia ya kurasa za nyaraka zilikuwa zimewekwa kwenye mtandao wa kijamii wa Discord na mtu ambaye alikuwa akifanya kazi katika kambi ya kijeshi ya Marekani.

Gazeti jingine la The New York Times, liliripoti kwamba nyendo za ushahidi wa kidijitali zinaonyesha Teixeira kama kiongozi wa kundi la mtandao wa Discord, linaloitwa Thug Shaker Central, ambako hati hizo zilivujishwa.

Tukio hilo liloelezwa kuwa la aibu la kuvuja kwa taarifa za kiusalama, zinazohusisha nyaraka nyeti, limeleta wasiwasi kwa Marekani kuhusu uwezekano wa uvamizi nchini Ukraine kupambana na wanajeshi wa Russia.

**DW**

# Watu 11 wafariki kwa kufunga, wakitaka kukutana na Yesu

**NAIROBI,** KENYA

WATU wanne wamefariki dunia na wengine zaidi ya kumi wamelazwa katika hospitali ya kaunti ya pwani ya Kilifi nchini Kenya, baada ya kufunga kwa lengo la kukutana na Yesu.

Polisi nchini humo walisema kundi hilo lilipatikana katika msitu walimokuwa wakiishi kwa siku kadhaa baada ya kuambiwa na mhubiri wa eneo hilo kufunga huku "wakingoja kukutana na Yesu".

Mamlaka ilisema iliokoa watu 11, kati ya hao sita walikuwa wamedhoofika na kuwa na hali mbaya ya afya.

Maofisa wa pilisi walisema wataanza tena msako wa kuwatafuta wanachama zaidi wa kundi hilo Ijumaa asubuhi kufuatia ripoti kwamba wengine walikuwa bado wako msituni.

Polisi wanaripotiwa kugundua kaburi ndani ya msitu huo ambalo pia litachunguzwa.

Watu hao ni waumini wa Kanisa la Good News International Church, linaloongozwa na mchungaji wa eneo hilo ambaye amekuwa akichunguzwa na polisi kwa madai ya kuwataka waumini wake kufa njaa ili kufika mbinguni kwa kasi.

Kwa sasa muhubiri huyo yuko huru baada ya kuachiliwa kwa dhamana ya polisi baada ya kushtakiwa mwezi uliopita kutokana na vifo vya watoto wawili ambao wazazi wao ni miongoni mwa wafuasi wake.

**BBC**

# HADITHI

MBWA mmoja wa jirani wa maeneo ya Kinondoni Msisiri, alionekana kuvutiwa na kiroba kilichotupwa upenuni mwa nyumba moja. Ni moja kati ya viroba ambavyo hutupwa usiku au alfajiri na vijana wanaokusanya taka kwenye nyumba za watu na kupewa ujira kidogo. Wao badala ya kwenda kutafuta maeneo ya kutupa, hupita vichochoroni na kama hajaonekana anautupa mzigo na kuendelea na safari yake. Ilitokea kwenye nyumba moja huko, na mbwa huyo alipouvuta, kiungo vya mwili wa bianadamu vilianguka. Majirani a kwanza kuona walipiga kelele na watu wakajazana. Akinamama wakiangua vilio. Viungo vilihifadhiwa kwa kufunikwa. Polisi walianza msako. Kwa kuanzia tu wakaanza kuwakamata wazoa taka na waokota chupa za kwenda kuuza, wote wa maeneo hayo na jirani wanaofahamika tayari kwa mahojiano na uchunguzi, wakihisiwa kuwa huenda mmoja wao au zaidi kuhusika na mauaji. Ni maiti ya nani? Na Muuaji ni nani? Fuatilia mwanzo hadi mwisho kujua mkasa mzima ulivyokuwa.

# MAITI KWENYE KIROBA-4

**Na Adam Fungamwango : (0716 350534)**

"Mama Miraji huyo. Mama Miraji ndiye aliyeniambia, alfajiri anasikia mbwa analia nje ya dirisha lake. Mbwa haondoki, ikabidi atoke na mumewe wamfukuze na mawe. Lakini asubuhi, akaitwa na watu waliokuwa nje. Walikuwa wanamuona mbwa akivuta kiroba, akakichana ndiyo viungo vya binadamu vilipoonekana. Baadaye nikaitwa na mimi mwenye nyumba. Ndivyo ilivyokuwa."

"Umejibu vema bibi, labda unaweza kuniambia unahisi ni nani aliyekuja kuweka kiroba cha maiti upenuni mwa nyumba yako?"

"Baba, nadhani hawa hawa vijana wanaopita kukusanya taka kwenye nyumba za watu."

"Lakini bibi, kwenye mitaa si kuna magari maalum yanakuja kuchukua takataka kila mwezi na mnalipia serikali za mitaa? Kwa nini mnaruhusu watu tu wengine wanakuja kuchukua?"

"Baba, wakati mwingine hawa watu wa magari ya taka hawaji hata miezi miwili, na sisi tunahifadhi kwenye viroba na kila mtu na utumiaji wake, wengine wako wachache, wengine familia zao kubwa, wengine wanazalisha taka nyingi kuliko wengine. Kwa hiyo wakiona zimejaa, wanapita vijana hawa wanawapa pesa, wanabeba viroba na kuondoka navyo." Bi. Mkali aliendelea kujibu maswali ya Sajenti Moses kwa ufasaha.

"Huwa wanakwenda kutupa wapi? Kuna dampo ambalo huwa wanakwenda kutupa?"

"Hapo sasa. Ndiyo maana utakuta kuna siku kiroba kimoja au viwili vimetelekezwa hapo upenuni. Yaani hawa wanachofanya wakichukua taka, wanakwenda kweli sehemu fulani ambazo taka zitatupwa labda mtoni, lakini mara nyingi viroba vya hapa watakwenda kuvitelekeza huko mbali kabisa na hapa. Na vya huko vitaletwa huku. Leo upenuni kwa nyumba yangu, kesho nyumba zingine huko mbele, yaani haya baba ndiyo maisha ya watu huku uswahilini na tumeshayazoea wenyewe."

Baada ya maswali kadhaa Sajenti Moses aliridhika na majibu ya Bi Mkali na sasa alimuuza kama anaweza kumpata mama Miraji.

Bibi akanyanyuka huku akigugumia kwa maumivu. Sajenti alimuonea huruma lakini hakuwa na namna. Angekuwa anamfahamu mama Miraji angekwenda kumwita yeye.




**"Ni watu gani ambao huwa wana tabia ya kutelekeza au kutupa viroba upenuni kwa nyumba zenu?"**

"Pole bibi." Akampoza.

"Ahsante, uzee huu mwanangu." Akajibu.

Akavuta hatua taratibu na kutoka nje.

Dakika nne baadaye alirejea akiwa ameongozana na mwanamke alimkadiria kuwa na miaka 27 hivi.

Alikuwa amevaa dela lake refu, akionyesha wajihi wa mama wa nyumbani ambaye hakuonyesha kwamba ana mpango wowote wa kutoka hapo kwenda sehemu nyingine kwa muda huo.

"Shikamoo." Akaamkia.

"Marahaba, mama, naomba ukae hapa."

Akakaa, lakini uso wake bado ulionyesha mshangao. Hakujua anaitiwa nini. Bi Mkali hakumwambia lolote zaidi ya kwamba kuna mtu yupo ndani kwake anamuomba.

Alipoingia na kumkuta mwanaume ambaye umri wake akaukadiria kuwa wa mtu mzima mwenye miaka 45 hivi, akili yake ikamtuma kuwa huenda ni mgeni wa bibi huyo ambaye amemuona huko nje na amemzimia, hivyo bibi ametumwa kama mshenga ili mambo yawe sawa.

"Mhh, nimkubalie baba huyu halafu baba Miraji akijua, itakuwaje? Bibi si anataka kunitafutia balaa huyu?" Akawaza mama Miraji.

"Wewe ndiye mama Miraji?" Sajenti akauliza huku akitabasamu.

"Ndiyo mimi." Akajibu kwa sauti ya kutengeneza ambayo huitumia kwa kumvuta mtu, lakini iliyochanganyikana na woga.

"Okay, mimi naitwa Sajenti Mosses, niko hapa kwa ajili ya uchunguzi wa kukutwa kwa kiroba chenye maiti upenuni wa nyumba yenu."

Hapo ndipo akili ya mama Miraji ilipokaa sawa. Hayakuwa mambo yale aliyokuwa akiyafikiria sekunde chache zilizopita.

Aliyekuwa mbele yake siyo baba mkware aliyemuona na kumtamani, bali ni askari polisi aliyevaa kiraia. Tena alikuwa akichunguza kifo cha mwanamke Tessy. Ambaye mwili wake ulikutwa ndani ya kiroba ukiwa umekatwakatwa viungo. Kiroba hicho kiliegeshwa kwenye nyumba ya Bi Mkali na mtu wa kwanza kufahamu hilo ni yeye.

"Niambie siku ya tukio ilikuwaje?"

"Nakumbuka kama saa kumi alfajiri hivi nilisikia mbwa anabweka nje ya dirisha langu, ikabidi mimi na mume wangu tutoke tukamfukuze kwa sababu ilikuwa kero, usingizi haupatikani tena. Tuliporudi kulala. Asubuhi ndiyo naitwa na mpita njia mmoja simkumbuki nani, akaniambia mbwa anavuta kiroba ambacho kilikuwa kama kuna damu imegandia. Nikaogopa ikabidi tuamshane. Tukaamsha na waume zetu, kwenda kuangalia kumbe alichokuwa anavuta ni viungo vya biandamu."

"Wewe unadhani ni nani au nini kimetokea kwenye hili?"

"Mimi bwana afande kwa akili yangu, mbwa alipokuwa analia nadhani itakuwa ndiyo wakati huyu mtu alikuwa amefika pake karibu na dirisha langu akakitelekeza kiroba."

"Ina maana kimewekwa hapo majira ya saa kumi alfajiri?"

"Itakuwa hivyo." Akajibu mama Miraji.

"Ni watu gani ambao huwa wana tabia ya kutelekeza au kutupa viroba upenuni kwa nyumba zenu?"

"Wazoa taka mitaani ndiyo wana tabia hii. Huwa inatukera ila basi tu."

Sajenti Mosses aliridhika na majibu ya mama Miraji pamoja na Bi Mkali, akawaaga na kuahidi kama kutakuwa na kitu cha ziada basi angerejea tena. Wakamuaga kwa bashasha kwa sababu hawakuona dalili yoyote ya wao kuhisiwa au kuambiwa kitu chochote kwamba kuna kitu walikosea kwenye tukio zima.

Kwa jinsi upelelezi wa muda mfupi tu ambao ameufanya, aliona kabisa kuwa wazoa taka ambao huwa wanapenda kutembea alfajiri kwa ajili ya kutelekeza viroba vya taka kwenye vichochoro vya nyumba za watu, au waokota chupa za plastiki ambao nao wana tabia ya kuamka alfajiri kwa ajili ya kuwahi chupa zilizotupwa usiku na watumiaji kwa ajili ya kwenda kuziuza, ndiyo waliohusika na tukio hili na si vinginevyo. Tayari alishatoa amri ya kukamatwa, kilichobaki ni kuwahoji ili kumpata muuaji.

**ITAENDELEA JUMAMOSI**

# BEKI WA KIMATAIFA YANGA KUIKOSA SIMBA SC KESHO

**Na Adam Fungamwango**

WAKATI ikitarajia kucheza mechi dhidi ya watani zao Simba kesho, Yanga itamkosa beki wake raia wa Mali, Mamadou Doumbia, kutokana na kufiwa na baba yake mzazi, imeelezwa.

**Taarifa iliyotolewa na Idara ya Habari na Mawasiliano ya Yanga jana, imesema Doumbia aliondoka nchini jana kuelekea kwao Mali kwa ajili ya kushiriki taratibu za mazishi, na hivyo ataukosa mchezo huo mkubwa.**

Mchezaji huyo ambaye alisajiliwa kipindi cha dirisha dogo, hakupata nafasi ya kucheza katika mechi kadhaa, kabla ya kupata nafasi hiyo kwenye mchezo uliopita wa Ligi Kuu Tanzania Bara dhidi ya Kagera Sugar.

"Klabu ya Yanga imepokea kwa masikitiko makubwa taarifa za kifo cha baba mzazi wa mchezaji wetu, Mamamou Doumbia, kilichotokea jana (juzi) nchini Mali.

Doumbia anatarajia kusafiri asubuhi leo (jana), kuelekea Mali kwa ajili ya taratibu za mazishi. Kwa niaba ya wanachama, wapenzi na mashabiki wa Yanga, uongozi wa Yanga unatoa pole kwa mchezaji wetu, Doumbia na familia yake yote kwa msiba huo na Mwenyezi Mungu awatie nguvu katika kipindi hiki kigumu." Ilimaliza sehemu ya taarifa hiyo ya klabu hiyo.

Hata hivyo, haitokuwa tatizo katika kikosi hicho kutokana na nyota huyo bado hajaingia kwenye mfumo wa kuaminiwa moja kwa moja, hivyo ukuta wa kati Yanga utaendelea kuongozwa na Dickson Job, Bakari Mwamnyeto, Ibrahim Abdallah 'Bacca' na Yannick Bangala.

Mabingwa hao watetezi wa Ligi Kuu Tanzania Bara, Yanga watashuka dimbani kuwavaa Simba wakiwa ndio vinara wa ligi hiyo na msimu hii ikiwa imetinga hatua ya robo fainali ya mashindano ya kimataifa ya Kombe la Shirikisho Afrika.

Pia itashuka katika mechi hiyo ikiwa na kumbukumbu ya ushindi mnono wa mabao 5-0 walioupata dhidi ya Kagera Sugar.

## Kili Marathon wamlilia Bayo

**Na Mwandishi Wetu**

WAANDAAJI wa mbio za kimataifa za Kilimanjaro Marathon wameeleza kuhuzunishwa kufuatia kifo cha Mkurugenzi wa mbio hizo, John Bayo, kilichotokea Jumanne jijini, Arusha baada ya kuugua kwa muda mrefu.

Taarifa iliyotolewa na waandaaji hao imesema marehemu Bayo alikuwa ni 'kiungo' mhimili muhimu katika mbio hizo maarufu hapa nchini.


"Mtu mwema kiasi hiki anapofariki, inakuwa vigumu sana kuzungumza, tumepoteza muhimili mkubwa mno katika Kilimanjaro Marathon na rafiki wa kipekee," ilisema taarifa hiyo ya waandaaji hao.

Bayo alikuwa mmoja wa waanzilishi wa mbio hizo zilizoanza kufanyika tangu mwaka 2003 ambapo washiriki wasiozidi 500 walikimbia kwa kujifurahisha lakini zaidi ya miaka 20 baadaye, mbio hizo zimevutia zaidi ya washiriki 12,000 kutoka zaidi ya mataifa 55.

"Alishirikiana pia na waandaaji wa mbio nyingine nchini Tanzania na kuwafundisha namna ya kuandaa mbio kwa weledi," iliongeza sehemu ya taarifa hiyo.

Mkongwe huyo mara kadhaa aliwataka wanariadha wa Tanzania kushiriki katika mbio mbalimbali nje ya nchi kwa lengo la kujitangaza na kukuza vipaji vyao.

"Kwetu sisi alikuwa kama ndugu, mstaarabu na hodari katika kazi yake ambayo aliifanya kwa weledi mkubwa, tutamkumbuka mno."





Mchezaji wa kimataifa wa Azam FC, Issa Ndala (kushoto), akijiandaa kumtoka, Rodger Kola katika mazoezi ya timu hiyo kwa ajili ya kujiandaa na mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara dhidi ya Ruvu Shooting itakayochezwa Aprili 22, mwaka huu kwenye Uwanja wa Jamhuri, Morogoro. **PICHA: AZAM FC**

## Riadha kuelekea Zambia Aprili 24

**Na Shufaa Lyimo**

TIMU ya Taifa ya riadha ya vijana wenye umri chini ya miaka 18 na 20 itaondoka nchini Aprili 24, mwaka huu kuelekea Zambia kwa ajili ya kushiriki mashindano ya Afrika, imeelezwa jijini, Dar es Salaam jana.

Mashindano ya riadha ya Afrika kwa vijana chini ya umri yanatarajia kufanyika kuanzia Aprili 27 hadi Mei 3, mwaka huu nchini humo.

Mjumbe wa Kamati ya Utendaji ya Shirikisho la Riadha Tanzania ( RT), Felix Chunga, alisema wanariadha hao wanaendelea vizuri na mazoezi na wanatarajia wataenda kuitangaza vyema bendera ya nchi katika mashindano hayo.

"Tunafahamu mashindano hayo yatakuwa na upinzani mkubwa, tunaomba wadau mbalimbali waiunge mkono timu hii ili tutimize malengo yetu," alisema Chunga.

Aliongeza RT bado itaendelea kumkumbuka aliyewahi kuwa Makamu Mwenyekiti wa RT, John Bayo, ambaye alifariki dunia Jumanne akiwa jijini Arusha baada ya kuugua kwa kipindi kirefu.

## CHAMUDATA na Ukatili wa Kijinsia

**Na Sabato Kasika**

BENDI inayoundwa na wanamuziki wanawake ikiwa chini ya umiliki wa Chama cha Muziki wa Dansi Tanzania (CHAMUDATA), imekamilisha wimbo unaohamasisha vita dhidi ya vitendo vya ukatili wa kijinsia.

Akizungumza na gazeti hili jijini Dar es Salaam jana, Mwenyekiti wa CHAMUDATA (Wanawake), Deborah Nyangi, aliutaja wimbo huo mpya unaitwa Tanzania bila ukatili wa kijinsia inawezekana.

"Tumeamua kutumia sanaa kutoa elimu kuhusu ukatili wa jinsia, kuna matukio mengi ya ukatili huo ndani ya jamii, hivyo nasi kama sehemu ya kioo cha jamii hatuna budi kutoa mchango wetu," alisema Deborah.

Alisema tayari wamekamilisha video ya wimbo huo na watapanga ratiba ya kutembelea shule mbalimbali na katika kumbi za starehe kuutambulisha ikiwa ni sehemu ya kuhamasisha vita ya kutokomeza ukatili huo.

Aliongeza bendi hiyo inaundwa na wanamuziki 15 na baadhi yao ni Anna Mwaole, Luiza Mbutu, Khadija Kimobitel, Anneth Kushaba, Tabu Mambosasa, Getrude Joseph, Sarah Sauti na Taji Mbaraka.

## ZISIKUPITE

**BAYERN YAMTAKA KANE**
KLABU ya Bayern Munich imeonyesha nia ya kumsajili mshambuliaji wa Timu ya Taifa ya England, Harry Kane, mwenye umri wa miaka 29 kutoka Tottenham msimu huu wa joto, hata hivyo Manchester United wapo mstari wa mbele kumnyakua mchezaji huyo kwa sababu anataka kusalia katika Ligi Kuu England. (***Mirror***)

**ALISTER ANUKIA LIVERPOOL**
KLABU za Liverpool, Chelsea na Manchester United zimeonyesha nia ya kumsajili kiungo wa kati wa Brighton na Timu ya Taifa ya Argentina, Alexis Mac Allister, mwenye umri wa miaka 24, ambaye atafurahia uhamisho wa majira ya joto. (***Guardian***)

**JAMES ATAKIWA MADRID**
REAL Madrid iko tayari kuwasilisha ombi jipya la kutaka kumsajili beki wa England, Reece James mwenye umri wa miaka 23, iwapo Chelsea italazimika kuuza wachezaji msimu huu wa joto. (***Mail***)

**NAGELSMANN NA CHELSEA**
ALIYEKUWA Kocha wa Bayern Munich, Julian Nagelsmann, mwenye umri wa miaka 35 amepokea wito wa kukutana na bodi ya Chelsea huku klabu hiyo ikiendelea kutafuta kocha mpya wa kudumu. Bosi wa zamani wa Hispania, Luis Enrique (52), tayari amefanya mazungumzo na timu hiyo (***Bild***)

**MBAPPE ATAKA UEFA**
MSHAMBULIAJI wa Ufaransa, Kylian Mbappe mwenye umri wa miaka 24 amesema lengo lake ni kushinda Ligi ya Mabingwa Ulaya akiwa na Paris St-Germain, licha ya mwaka jana kukaribia kuondoka katika klabu hiyo na kuelekea Real Madrid. (***90min***)

**FATI AIKATAA UNITED**
MSHAMBULIAJI wa Hispania, Ansu Fati mwenye umri wa miaka 20 anataka kusalia Barcelona, licha ya kutakiwa na Bayern Munich, Manchester United na Tottenham . (***Mundo Deportivo***)

**AC MILAN KUJIIMARISHA**
AC Milan wamemwongeza mshambuliaji wa England (U-21), Folarin Balogun, ambaye yuko kwa mkopo Reims kutoka Arsenal, kwenye orodha ya wachezaji wanaolengwa katika majira ya joto. (***Calciomercato***)

**CAICEDO AINGIA SOKONI**
KLABU ya Manchester United pia imemweka kiungo wa kati wa Brighton na Timu ya Taifa ya Ecuador, Moises Caicedo, mwenye umri wa miaka 21 kwenye orodha yao fupi ya uhamisho. (***Telegraph***)

**DISASI ATAJWA CITY**
KLABU za Manchester City na Chelsea zote zilituma maskauti kumtazama mlinzi wa Monaco, Axel Disasi, mwenye umri wa miaka 25 wikendi iliyopita. (***Le Parisien***)

**URIBE KUTUA FULHAM**

KLABU ya Fulham inafikiria kumnunua kiungo wa kati wa Porto wa Colombia, Mateus Uribe mwenye umri wa miaka 32 kuichukua nafasi ya mchezaji wa kimataifa wa Ureno, Joao Palhinha (27), ambaye analengwa na Manchester United . (***Sun***)

**RODRIGUEZ AONDOKA UGIRIKI**

KIUNGO wa kati wa Colombia, James Rodriguez, mwenye umri wa miaka 31 ni mchezaji huru baada ya kukubali kusitisha mkataba na klabu ya Olympiacos ya Ugiriki (***Liverpool Echo***)

# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA



# BAYERN MUNICH YAMFUNGIA MANE

**MUNICH,** Ujerumani

### Ni kutokana na kosa la utovu wa nidhamu aliloonyesha dhidi ya nyota...

SADIO Mane amefungiwa na kupigwa faini na klabu yake ya Bayern Munich baada ya kudaiwa kumpiga ngumi mchezaji mwenzake, Leroy Sane.

**Fowadi huyo wa zamani wa Liverpool alionekana akibishana na Sane wakati Bayern Munich ilipochapwa mabao 3-0 katika mechi ya kwanza ya robo fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya dhidi ya Manchester City iliyochezwa Jumanne.**

Ripoti zimedai mshambuliaji huyo wa Timu ya Taifa wa Senegal alimpiga mdomoni winga huyo wa Ujerumani mara baada ya mchezo huo kumalizika.

Wawili hao waliripotiwa kuomba msamaha mbele ya wenzao kwenye mazoezi siku ya Alhamisi, lakini Bayern Munich walithibitisha Mane hatakuwapo katika kikosi cha mechi ya nyumbani dhidi ya Hoffenheim itakayochezwa leo.

Taarifa kutoka kwa mabingwa hao wa Bundesliga iliyotolewa juzi ilisema Mane hatahusika wikendi hii kutokana na "utovu wa nidhamu" kufuatia baada ya kupoteza mechi kwenye Uwanja wa Etihad.

Inadaiwa Mane alimpiga Sane, ambaye pia ana asili ya Senegal baada ya kumwonyesha vitendo vya kibaguzi jambo ambalo lilimuumiza zaidi nyota huyo mwenye kuaminika kwamba ni mtulivu.

Mane ana mabao 11 na asisti tano katika mechi 32 msimu huu, huku Sane akiwa na mabao 13 na asisti saba katika mechi 36 alizocheza tangu alipotua Ujerumani.

SCAN HAPA KUPAKUA APP YETU!
SUPA JACKPOT KWA 1000/- 1,102,0

JACKPOT
MECHI WIKI HII
TAREHE: 19,20 NA 21 APRILI 2023
BASHIRI KWA USAHIHI MECHI ZOTE 13

| TAREHE | MUDA | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 01. 19/04/23 | 17:00 | Istanbulspor vs Antalyaspor | 2.73 | 3.31 | 2.40 |
| 02. 19/04/23 | 17:00 | Kayserispor vs Kasimpasa | 2.31 | 3.35 | 2.83 |
| 03. 19/04/23 | 18:00 | Fotbal Trinec vs Pribram | 2.68 | 3.09 | 2.42 |
| 04. 19/04/23 | 20:30 | Konyaspor vs Adana Demirspor | 2.61 | 3.30 | 2.51 |
| 05. 19/04/23 | 21:45 | Blackburn vs Coventry | 2.30 | 3.15 | 2.95 |
| 06. 19/04/23 | 21:45 | Swansea vs Preston | 2.44 | 3.16 | 2.76 |
| 07. 19/04/23 | 22:00 | Bayern Munchen vs Manchester City | 2.54 | 3.41 | 2.48 |
| 08. 20/04/23 | 20:30 | Sivasspor vs Trabzonspor | 2.61 | 3.30 | 2.51 |
| 09. 20/04/23 | 22:00 | Sporting Lisbon vs Juventus | 2.34 | 3.17 | 2.97 |
| 10. 21/04/23 | 01:00 | San Lorenzo vs Fortaleza CE | 2.21 | 3.17 | 3.43 |
| 11. 21/04/23 | 05:00 | Universitario vs Goias | 2.23 | 3.12 | 3.01 |
| 12. 21/04/23 | 05:00 | Deportes Tolima vs CA Tigre | 2.27 | 3.28 | 3.17 |
| 13. 21/04/23 | 19:00 | Apollon Limassol vs Pafos FC | 2.44 | 3.27 | 2.74 |

KUWEKA PESA:
- PIGA *150*87#, CHAGUA 4
- WEKA PESA.

tigo pesa
vodacom m-pesa
halopesa
airtel money
SEND

SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
PIGA *150*87#
GBT:0249
18+
HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, PIGA:
0764115588, 0677115588
0685115588
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa

# JANGA LA MAJERUHI LAIKUMBA UNITED



**MANCHESTER,** England

KLABU ya Manchester United inakabiliwa na tatizo la majeruhi kabla ya kumalizika kwa msimu huu baada ya Lisandro Martinez na Raphael Varane kuumia katika sare ya mabao 2-2 dhidi ya Sevilla hapo juzi usiku.

Varane alitoka nje kabla ya mapumziko na Martinez alitolewa nje kwa machela dakika za majeruhi.

Sevilla walifunga mabao mawili ya dakika za lala salama na Ten Hag anakabiliwa na matatizo ya uteuzi wa safari ya Nottingham Forest Jhapo kesho huku Marcus Rashford, Luke Shaw, Scott McTominay, Alejandro Garnacho na Donny van de Beek wakiwa tayari nje ya uwanja.

Martinez alionekana kukosa raha wakati akiondoka uwanjani, ingawa Ten Hag alikanusha nyota huyo alikuwa ameumia sana.

"Sio eneo hilo, siwezi kujua ni nini lakini sio eneo la kifundo cha mguu," alisema Ten Hag.

"Nadhani hatacheza Jumapili. Inaonekana hivyo lakini siwezi kusema utambuzi ni nini na napendelea kungoja niseme ni nini.

"Tuna mbadala wazuri sana wa Harry Maguire, Victor Lindelof na Luke Shaw. tuna wachezaji ambao wanaweza kuchukua nafasi zao Martinez na Varane."

United walifunga mabao mawili katika dakika 20 za mwanzo dhidi ya Sevilla kupitia kwa Marcel Sabitzer huku timu ya Ten Hag ikidhibiti mchezo.

Lakini matokeo duni kipindi cha pili yalimalizika kwa Tyrell Malacia na Maguire kufunga mabao ya kujifunga wenyewe katika dakika sita za mwisho na kuwafanya Wahispania hao wafuzu kwa mkondo wa pili nchini Uhispania wiki ijayo.

# Vinicius ampeleka Ancelotti Brazil



**MADRID,** Hispania

MCHEZAJI Vinicius Junior alimsifu Carlo Ancelotti kama kocha bora zaidi duniani baada ya Real Madrid kushinda mabao 2-0 dhidi ya Chelsea katika mchezo wao wa robo fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya, akiongeza anatumani Mtaliano huyo anaweza kumfundisha klabu na nchi.

Ancelotti, ambaye amekuwa akihusishwa mara kwa mara kuchukua kazi iliyoachwa wazi ya timu ya taifa ya Brazil msimu huu, ana mkataba wa Madrid hadi mwaka 2024.

Amepata shinikizo baada ya kuanguka kwa pointi 13 nyuma ya Barcelona katika mbio za kuwania taji la LaLiga, licha ya kuiongoza Madrid kutinga robo fainali ya Ligi ya Mabingwa na fainali ya Copa del Rey.

"Hebu tumaini ni wote wawili!" Vinicius alisema, akicheka, alipoulizwa na waandishi wa habari kama angependelea Ancelotti kama kocha wa Madrid au Brazil.

"Kwangu mimi, ndiyo yeye ni kocha bora zaidi duniani. Sijui kuhusu kila mtu, lakini kwangu na kwa wachezaji wa hapa, yuko."

Vinicius amechangia katika kufunga mabao 20 katika mechi 20 zilizopita za Ligi ya Mabingwa Ulaya, akiwa amefunga mabao 10 na asisti 10, likiwemo la mshindi katika fainali ya mwaka jana.

82,037/-

# SERIKALI, YANGA ZAUNGANA KUPIGA VITA UKATILI KIJINSIA

**Na Saada Akida**

WAZIRI wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum, Dk. Dorothy Gwajima, amezitaka Simba, Yanga, na vyama vya michezo kushirikiana na serikali katika kupiga vita vitendo vya ukatili wa kijinsia kwa wanawake na watoto.

**Dorothy aliyasema hayo jana wakati akiwatambulisha rasmi Yanga kuwa mabalozi wa kupinga na kutokomeza ukatili wa kijinsia hapa nchini.**

Alisema, karne ya sasa michezo imekuwa mstari wa mbele na kufuatiliwa na watu wengi, ninaimani ushirikiano na Yanga watafikia malengo ya kupinga mmomonyoko wa maadili hasa wa kijinsia.

Alisema mmong'onyoko wa maadili ni agenda kubwa na kufanyiwa kazi na serikali, wasipokuwa makini tutakuwa na watu wasiokuwa na nidhamu kuanzia nyumbani hadi katika michezo.

"Ili kuleta maendeleo ya taifa lazima tulinde watu wetu hasa ukatili wa kijinsia, klabu ya Simba na timu nyingine za michezo kujitokeza kama ilivyo kwa Yanga kushirikiana na wizara kupiga vita ukatili. Ushirikiano rasmi na Yanga umeanza kufungua njia kwa wengine kuja katika agenda ya kitaifa," alisema Dorothy.

Naye Rais wa Yanga, Hersi Said, alisema wameamua kuunga mkono juhudi za serikali, katika kupiga vita vitendo vya ukatili kwa kijinsia hasa wengi wao wakiwa ni mashabiki wa michezo.

"Tusipowalinda wanawake na watoto basi mashabiki hao tutawapoteza, ipo siku uwanjani hatutakuwa na mashabiki kabisa kwa sababu hatukuwalinda. Tukumbuke zamani watoto na wanawake hawakuruhusiwa kwenda uwanjani kwa sababu ya kuonekana sehemu ya kiuni, ila sasa tunaona jinsi gani hao watu wanavyokuja uwanjani, Yanga tumeungana na wizara kuhakikisha tunawalinda mashabiki na wachezaji wetu," alisema Hersi.



## *Simba, Yanga zachanga karata*

INATOKA UK 24

Simba yenyewe itashuka katika dabi hiyo ikimtumia kwa mara ya kwanza ni Jean Baleke, straika wa kumainiwa kwa sasa na timu hiyo, Saido Ntibazonkiza ambaye ameshawahi kucheza dabi, lakini itakuwa ni ya kwanza akiwa na Wekundu wa Msimbazi pamoja na nyota, Clatous Chama, Pape Sakho na Kibu Denis.

## Fei Toto : Muda ukifika nitasema

INATOKA UK 24

zisimamiwe, tusiruhusu maharamia wanaotumia fedha. Hii si kwa Yanga tu, ni klabu zote," alisema mkurugenzi huyo.

Aliongeza Yanga wanataka kuona sheria na taratibu zinafuatwa, kamwe hawawezi kumruhusu aondoke kiholela kwa maslahi ya heshima ya klabu.

"Yanga ilitoa taarifa kama kuna timu inamhitaji nyota huyo basi wafike katika ofisi zetu na Fei Toto mwenye aje kukaa meza moja ili kuvunja huo mkataba," aliongeza.

Nyota aliwasilisha shauri la kutaka kuvunja mkataba wake na Yanga kwa kulipa kiasi cha Sh. milioni 112 kama mkataba wake ulivyosema, lakini klabu hiyo ilikataa na kufungua kesi TFF.


# SUPA JACKPOT
# MECHI WIKI HII

BASHIRI KWA USAHIHI MECHI ZOTE

| TAREHE | MUDA | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 01. 15/04/23 | 17:00 | Wolverhampton Wanderers vs Brentford FC | 2.33 | 3.10 | 2.95 |
| 02. 15/04/23 | 17:00 | Chelsea FC vs Brighton & Hove Albion | 2.41 | 3.25 | 2.75 |
| 03. 15/04/23 | 17:00 | Southampton FC vs Crystal Palace | 2.60 | 3.10 | 2.60 |
| 04. 15/04/23 | 17:00 | Blackpool vs Wigan Athletic | 2.35 | 3.05 | 3.00 |
| 05. 15/04/23 | 17:00 | Queens Park Rangers vs Coventry City | 2.90 | 3.00 | 2.41 |
| 06. 15/04/23 | 17:00 | Stoke City vs West Bromwich Albion | 2.55 | 3.10 | 2.65 |
| 07. 15/04/23 | 17:00 | KAS Eupen vs SV Zulte Waregem | 2.33 | 3.40 | 2.75 |
| 08. 15/04/23 | 17:30 | Estoril Praia vs Portimonense SC | 2.38 | 3.00 | 3.00 |
| 09. 15/04/23 | 18:00 | Stade Rennes vs Stade Reims | 2.22 | 3.30 | 2.95 |
| 10. 15/04/23 | 19:15 | KV Oostende vs Oud-Heverlee Leuven | 2.48 | 3.45 | 2.50 |
| 11. 15/04/23 | 22:00 | Sparta Rotterdam vs SC Heerenveen | 2.23 | 3.30 | 2.95 |
| 12. 15/04/23 | 22:00 | America FC MG vs Fluminense FC RJ | 2.70 | 3.10 | 2.55 |
| 13. 16/04/23 | 00:30 | Botafogo FR RJ vs Sao Paulo FC SP | 2.49 | 3.05 | 2.80 |
| 14. 16/04/23 | 03:30 | Gimnasia Y Esgrima La Plata vs CA Belgrano | 2.30 | 2.75 | 2.90 |
| 15. 16/04/23 | 19:30 | Malaga CF vs FC Cartagena | 2.31 | 2.90 | 3.20 |
| 16. 16/04/23 | 20:00 | Union de Santa Fe vs CA Tigre | 2.60 | 2.85 | 2.47 |
| 17. 16/04/23 | 20:30 | VfL Wolfsburg vs Bayer Leverkusen | 2.75 | 3.35 | 2.32 |

# MECHI ZA USHINDI

"1" NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA "X" NI TIMU KUTOKA SARE "2" NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

## JUMAMOSI - 15/04/2023

| MUDA | GAME ID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 12:45 | 5812 | Western Sydney vs Melbourne Victory | 2.17 | 3.26 | 3.16 |
| 14:00 | 5338 | Dinamo Moscow vs Nizhny Novgorod | 1.51 | 3.97 | 5.64 |
| 14:00 | 5707 | Shakhter Karagandy vs Maktaaral | 2.67 | 3.03 | 2.47 |
| 14:30 | 1745 | Aston Villa vs Newcastle | 3.35 | 3.25 | 2.06 |
| 14:30 | 3697 | Hibernian vs Hearts | 2.24 | 3.26 | 3.01 |
| 15:00 | 1422 | Villarreal vs Valladolid | 1.40 | 4.59 | 6.39 |
| 16:00 | 2033 | Zesco United vs Zanaco | 1.74 | 2.93 | 5.15 |
| 16:00 | 3030 | Istanbulspor vs Basaksehir | 4.09 | 3.46 | 1.81 |
| 16:00 | 3250 | Bologna vs AC Milan | 2.95 | 3.05 | 2.36 |
| 16:00 | 3775 | Red Arrows vs Prison Leopards | 2.09 | 2.82 | 3.59 |
| 16:30 | 1993 | RB Leipzig vs Augsburg | 1.22 | 5.82 | 9.84 |
| 16:30 | 3359 | Gaborone United vs Masitaoka FC | 1.42 | 3.80 | 6.00 |
| 16:30 | 3654 | Sochi vs FC Krasnodar | 2.40 | 3.35 | 2.67 |
| 16:30 | 3681 | FC Koln vs Mainz | 2.55 | 3.20 | 2.60 |
| 16:30 | 5226 | Bayern Munchen vs Hoffenheim | 1.23 | 6.09 | 8.79 |
| 16:30 | 5512 | Stuttgart vs Borussia Dortmund | 3.34 | 3.64 | 1.94 |
| 17:00 | 1045 | Everton vs Fulham | 2.02 | 3.25 | 3.50 |
| 17:00 | 1869 | Wolverhampton vs Brentford | 2.38 | 3.09 | 2.89 |
| 17:00 | 1977 | Southampton vs Crystal Palace | 2.65 | 3.05 | 2.60 |
| 17:00 | 2222 | BSC Young Boys vs SC Bruhl | 2.31 | 3.50 | 2.36 |
| 17:00 | 3370 | Swansea vs Huddersfield | 1.69 | 3.59 | 4.59 |
| 17:00 | 4147 | Livingston vs St Johnstone | 2.20 | 3.17 | 3.17 |
| 17:00 | 4459 | Tottenham vs Bournemouth | 1.44 | 4.39 | 5.99 |
| 17:00 | 4858 | Chelsea vs Brighton | 2.57 | 3.22 | 2.57 |
| 17:00 | 5336 | Motherwell vs Dundee Utd | 1.96 | 3.28 | 3.73 |
| 17:00 | 5643 | Stoke City vs West Bromwich | 2.20 | 3.15 | 3.15 |
| 17:00 | 5801 | Rangers vs St Mirren | 1.20 | 5.86 | 12.12 |
| 17:15 | 2982 | Athletic Bilbao vs Real Sociedad | 2.19 | 3.06 | 3.26 |
| 18:00 | 3125 | Rennes vs Reims | 2.18 | 3.41 | 2.95 |
| 18:00 | 3900 | NK Osijek vs Lokomotiva Zagreb | 2.15 | 3.18 | 3.03 |
| 19:00 | 1570 | Napoli vs Verona | 1.56 | 3.69 | 5.68 |
| 19:00 | 3809 | Servette Geneva vs FC Lugano | 2.14 | 3.26 | 3.21 |
| 19:00 | 3884 | Viking vs Lillestrom | 2.20 | 3.37 | 3.00 |
| 19:00 | 5483 | Torpedo Moscow vs Spartak Moscow | 6.91 | 4.50 | 1.38 |
| 19:15 | 1508 | Cercle Brugge vs St Truiden | 1.66 | 3.76 | 4.61 |
| 19:30 | 2897 | Manchester City vs Leicester | 1.18 | 6.35 | 11.47 |
| 19:30 | 3472 | Betis vs Espanyol | 1.80 | 3.39 | 4.19 |
| 19:30 | 5462 | Eintracht Frankfurt vs Monchengladbach | 1.70 | 3.89 | 4.09 |
| 19:45 | 1751 | Waalwick vs Groningen | 1.90 | 3.46 | 3.66 |
| 20:00 | 1908 | GD Chaves vs Benfica | 8.40 | 5.40 | 1.28 |
| 20:10 | 5215 | Dinamo Zagreb vs Slaven Belupo | 1.25 | 5.02 | 9.02 |
| 21:15 | 3089 | NK Celje vs Tabor Sezana | 1.47 | 3.95 | 5.74 |
| 21:30 | 5686 | FC Luzern vs FC Zurich | 2.36 | 3.37 | 2.74 |
| 21:45 | 1015 | Sligo Rovers vs Drogheda Utd | 1.80 | 3.33 | 3.95 |
| 21:45 | 2849 | Inter vs Monza | 1.42 | 4.29 | 6.59 |
| 22:00 | 1623 | Cadiz CF vs Real Madrid | 5.13 | 3.89 | 1.57 |
| 22:00 | 1995 | Paris St Germain vs Lens | 1.71 | 3.91 | 4.01 |
| 22:00 | 2918 | Sparta Rotterdam vs Heerenveen | 2.24 | 3.18 | 3.04 |
| 22:00 | 4446 | America Mineiro MG vs Fluminense | 2.82 | 3.12 | 2.36 |
| 22:30 | 2514 | Porto vs Santa Clara | 1.10 | 7.84 | 19.09 |

CHEZA KWA WAJIBU. KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.

# Michezo

Nipashe Jumamosi Aprili 15, 2023



Bayern Munich yamfungia Mane UK. 21




Rais wa Yanga, Injinia Hersi Said (kulia), akizungumza baada ya klabu yao kutambulishwa kuwa balozi wa kupambana na vitendo vya ukatili wa kijinsia kwa wanawake na watoto. Kushoto ni Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum, Dk. Dorothy Gwajima. **PICHA: MTANDAO**

## Fei Toto : Muda ukifika nitasema

**Na Saada Akida**

WAKATI uongozi wa Yanga ukimwita mezani kiungo, Feisal Salum 'Fei Toto' ili kumaliza sakata lake, nyota huyo amesema muda sahihi ukifika ataweka wazi mambo yote yanayoendelea kuhusiana na uamuzi wa kutaka kuachana na klabu hiyo ambayo ameufanya.

Fei Toto amesema hivyo jana ikiwa ni siku mbili zimepita baada ya Kamati ya Sheria na Hadhi za Wachezaji ya Shirikisho la Soka Tanzania (TFF) kusema itatoa uamuzi wake ifikapo Mei 4, mwaka huu.

Kiungo huyo aliliambia gazeti hili kwa sasa anasubiri kamati imalize kikao chake na kutoa hukumu, lakini muda muafaka ukifika atazungumza mambo yote muhimu hadharani.

"Muda ukifika nitazungumza, muda sahihi ukifika nitaweka kila kitu wazi," Fei Toto alisema kwa kifupi.

Naye Mkurugenzi wa Sheria wa Yanga, Simon Patrick, amesema wanamkaribisha mchezaji huyo kufanya mazungumzo na si kupitia njia nyingine tofauti.

Simon alisema Yanga hawamng'ang'anii nyota huyo lakini wanataka utaratibu ufuatwe, wakiruhusu mchezaji kuondoka kwa njia hii hakutakuwa mpira kwa sababu kila mchezaji ataamka asubuhi na atasema hana furaha basi anaondoka.

"Huu ni uhuni, hautakiwi kuruhusiwa katika mpira wetu, ziko njia rasmi za kuvunja mkataba na zinafahamika hadi Shirikisho la Soka Ulimwenguni (FIFA), tunachotaka kanuni za mpira

INAENDELEA UK 23

# Simba, Yanga zachanga karata

## Makocha waendeleza tambo, umakini na kutobweteka silaha muhimu...

**Adam Fungamwango na Saada Akida**

MUDA utazungumza, ndicho kilichobakia kuelekea mechi ya marudiano ya Ligi Kuu Tanzania Bara kati ya Simba na Yanga itakayochezwa kesho kuanzia saa 11:00 jioni kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam.

Makocha wa timu hizo, kila mmoja ametamba kikosi chake kiko tayari kwa mchezo huo unaosubiriwa kwa hamu na mashabiki wa soka ndani na nje ya Tanzania.

Kocha Msaidizi wa Yanga, Cedric Kaze, alisema jana wanajua mechi hiyo itakuwa ngumu, lakini watacheza kama fainali kwa ajili ya kuusaka ushindi na kujiimarisha kwenye mbio za kutetea ubingwa wanaoushikilia.

Kaze alisema wameisubiri sana mechi hiyo ya dabi na wao kama vinara wa ligi wanahitaji pointi tatu na si matokeo mengine licha ya kutambua mchezo huo utakuwa na ushindani unaotokana na ubora wa wapinzani wao.

Kocha huyo alisema wanajiandaa kufanya mabadiliko katika sehemu kubwa ya kikosi chao hasa kwenye safu ya ulinzi na hii inatokana na kuimarika kwa Simba katika siku za hivi karibuni.

" Tunafanya mazoezi kulingana na aina ya mechi tunaenda kucheza, tumekuwa na timu ambayo imekuwa inabadilika kila wakati, mabadiliko yatakuwapo katika maeneo mengi ikiwamo safu ya ulinzi ingawa siyo sasa naweza kutaja nani atakuwapo," alisema Kaze.

Aliongeza wataongeza umakini katika mechi hiyo itakayotoa mwanga wa mbio za ubingwa wa msimu huu lakini pia kujiweka imara kuelekea mechi yao ya robo fainali ya mashindano ya Kombe la Shirikisho Afrika.

Alisema pia hawataingia kwa kubweteka na rekodi, kwa sababu siku zote 'dabi' huwa haitabiriki.

"Ni mechi ambayo inasubiriwa na mashabiki wengi, tunajua nini cha kufanya, dabi siku zote haitabiriki, anayekuja kwa kupambana na kujituma, kufuata vizuri maelekezo ya walimu ndiyo anashinda, kuongoza kwetu ligi na nafasi tuliyonayo haitupi au kutusaidia lolote kupata ushindi, kitu kikubwa ni kujituma na kucheza kama fainali, hilo tunalijua na tupo tayari," Kaze alisema.

Naye Juma Mgunda alisema Simba imejipanga kucheza mechi hiyo kama fainali kwa sababu ndio utakaoamua hatima ya mbio za ubingwa kwa upande wao.

Mgunda alisema kikosi chao kilianza mazoezi mara baada ya kumaliza mechi dhidi ya Ihefu kwa sababu walifahamu wanahitaji kuwa imara zaidi katika kila eneo.

"Siyo kama tulianza maandalizi juzi, tulikuwa tunajua, na tarehe inafahamika kwa hiyo mechi hii tumejiandaa muda mrefu tu, hiki unachokiona ni tunakamilisha tu maandalizi ya mwisho ya mchezo. Tunaweza kusema mchezo ni mzito, tunaweza kusema una hatima yetu.

Vile vile kwa sababu bado tuko kwenye mbio za ubingwa na mimi huwa kila siku nasema 'haiwi mwisho hadi iwe mwisho', bingwa atapatikana baada ya ligi kumalizika. Tunaichukulia mechi hii kwa umuhimu wa kipekee kabisa," alisema Mgunda ambaye ndiye mwenyeji wa mechi hiyo.

Katika mechi hiyo, Yanga inajivunia ubora wa wachezaji wake wakiongozwa na Stephane Aziz Ki aliyefunga bao la kusawazisha kwenye mechi iliyopita, Fiston Mayele, straika tegemeo wa kikosi hicho, lakini pia wapo mawinga hatari kama Jesus Moloko na Tuisila Kisinda huku idara ya ulinzi ikiongozwa na Dickson Job, Bakari Mwamnyeto na Djuma Shaaban.

INAENDELEA UK 23

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >